# Nipashe

Jumatatu Mei 31, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580597

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Vikwazo** 30 vya biashara kati ya Tanzania, Kenya sasa vyaondolewa rasmi

UKURASA 3



**Mzee** Mwinyi asimulia alivyoruhusu kuanzishwa kwa shule za binafsi

UKURASA 3



**Alaba: Nasubiri kwa hamu kukipiga Madrid**

UKURASA 20



# Pangapangua ya Samia Ma-Ras

• **Wamo** maafisa wa Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu, balozi mstaafu, kigogo CCM... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 18

**HOMA YA NGURUWE BADO TISHIO NCHINI**

SERIKALI imesema ugonjwa wa homa ya nguruwe bado ni tishio...

UKURASA WA 18

**ASKARI WA UHAMIAJI WASIMAMISHWA KAZI**

IDARA ya Uhamiaji imewasimamisha kazi askari watatu wa Ofisi ya...

## Polisi wamkera Dk. Mwinyi kesi za udhalilishaji wa kijinsia

UKURASA 2



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (wapili kulia), Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe (wa tatu kulia) na Ofisa Mkuu wa wateja binafsi na Biashara Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wa tatu kushoto), wakizindua kwa pamoja Jukwaa la Vijana 'Go na NMB' lenye lengo la kutoa elimu ya kifedha pamoja na fursa za mikopo kwa vijana. Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Bei mafuta kula yauma, yapuliza

UKURASA 4

**MICHEZO** GOMES: UBINGWA NJIA NYEUPE SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Dk. Mwinyi achukizwa utendaji polisi kesi za udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hajaridhishwa na utendaji wa Jeshi la Polisi katika kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema yapo malalamiko kutoka kwa jamii kwamba jeshi hilo limekuwa likifanya upatanishi wa suluhu wa kesi hizo katika vituo vya polisi na kuzimaliza kienyeji.

Alikuwa akizungumza na wananchi pamoja na wanachama wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, jana makao makuu ya Chama Mkoa Amani mjini Unguja.

Alisema wanachokifanya polisi sio kazi yao kwa mujibu wa sheria kwa kuwa wanatakiwa kuhakikisha wanatayarisha kesi kwa kufanya upelelezi na kuzipeleka mbele kwa hatua nyingine na sio suluhu.

"Nilikutana na viongozi wa Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na mahakama na kuwataka wakutane na kuweka utaratibu mzuri utakaohakikisha kesi hizo zinasikilizwa haraka ili jamii iondokane na malalamiko," alisema.

Pia, Dk. Mwinyi aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya marekebisho mazuri katika sheria za udhalilishaji inayotaka mtuhumiwa wa makosa hayo asipewe dhamana.

"Nimemtaka Jaji Mkuu, sheria itekelezwa wanaofanya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwanza wanyimwe dhamana huku shauri lao likiendelea," alisema.

Alisema katika kipindi cha miezi sita ya uongozi wake amefanikiwa kujenga misingi ya maridhiano ya kisiasa ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Alisema kuwapo kwa SUK kumefungua milango ya maelewano ya kisiasa na kijamii na kuondokana na chuki huku zikiwamo kila aina ya dalili za matumaini yenye kheri.

Kadhalika, maandalizi ya ujenzi wa bandari za kisasa yenye ukubwa wa kilomita sita huko Mangapwani na Bumbwini upo katika hatua ya mwisho ambayo ni sehemu ya matarajio makubwa ya kutengeneza ajira nyingi. "Hapa wananchi na wanachama wengi wamezungumzia suala la serikali kuajiri vijana waliomaliza masomo yao...si kweli serikali haiwezi kuajiri vijana wote hao, lakini tunatengeneza mazingira ya ajira kwa kujenga miundombinu ya bandari na viwanda," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdala Juma Sadala, aliwataka watendaji wa chama hicho wakiwamo makatibu kujipanga kwa ajili ya kutekeleza ilani ya CCM kwa kufuatilia ahadi zote za serikali katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu.



Wafamasia kutoka Chama cha Wataalamu wa Famasia Tanzania (PST), wakipata maelezo kuhusu tangi la kuhifadhia maji kwa Mhandisi wa kiwanda cha dawa cha Kairuki Pharmaceuticals Industry Limited, Peter Luhwago, (juu kabisa) walipotembelea kujifunza mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Pangapangua ya Samia ma-RAS

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameendelea kufanya uteuzi wa viongozi mbalimbali katika serikali yake.

Safari huu amefanya uteuzi wa baadhi ya Makatibu Tawala wa Mikoa, kuwahamisha baadhi na wengine kuwabakisha katika vituo vyao vya kazi.

Kadhalika, Rais Samia Pia amefanya uteuzi wa viongozi wakuu wa taasisi za serikali.

**MAKATIBU TAWALA WA MIKOA**

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, Rais Samia amemteua Rodrick Mpogolo kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi. Kabla ya uteuzi huo, Mpogolo alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara.

Rais pia amemteua Dk. Athuman Juma Kihamia kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha. Kabla ya uteuzi huo, Dkt. Kihamia alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro.

Amemteua Hassan Abbas Rugwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kabla ya Uteuzi huo, Rugwa alikuwa Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi.

Dk. Fatuma Ramadhan Mganga ameteiliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma. Kabla ya uteuzi huo Dk. Mganga alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma.

Mussa Ramadhan Chogello ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita. Kabla ya uteuzi huo Chogello alikuwa Afisa katika Ofisi ya Rais.

Rais Samia Amemteua Ngusa Dismas Samike kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza. Kabla ya uteuzi huo Samike alikuwa Katibu wa Rais, Ikulu.

Mhandisi Mwanaisha Tumbo ameteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Mkoa wa Pwani. Kabla ya uteuzi huo Mhandisi Tumbo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Doroth Aidan Mwaluko ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida. Kabla ya Uteuzi huo Mwaluko alikuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu).

Balozi Batilda Salha Buriani ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. Kabla ya uteuzi huo Balozi Buriani aliwahi kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kenya na Japan.

Kadhalika, amemteua Azza Hilal Hamad kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu. Kabla ya uteuzi huo Azza aliwahi kuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga.

Pili Hassan Mnyema ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga. Kabla ya uteuzi huo, Mnyema alikuwa Afisa katika Ofisi ya Rais.

**WALIOHAMISHWA VITUO**

Rais Samia amemhamisha Dk. Seif Abdallah Shekillage aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro. Karoline Albert Mthapula aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara anakwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara.

Albert Gabriel Msovela aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga amehamishwa kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara. Angelina Mageni Lutambi aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida amehamIshwa kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya.

Mariam Amri Mtunguja aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya amehamishwa kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro. Abdallah Mohamed Malela aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi amehamishwa kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara.

Rais amemhamisha Judica Haikase Omari aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga kwenda Njombe. Denis Isdory Bandisa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita amehamishwa kwenda kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa wakati Missaile Albano Musa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara amehamishiwa Mkoa wa Songwe kuendelea kushika nafasi huyo.

**WANAOBAKI KATIKA VITUO VYAO**

Happiness William Seneda anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, huku Prof. Faustine Kamuzora anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera. Rashid Kassim Mchatta anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma.

Rehema Seif Madenge anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Steven Mashauri Ndaki anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma na Msalika Robert Makungu anabaki kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora.

**WATENDAJI WAKUU WA TAASISI**

Rais Samia amemteua William Erio kuwa Afisa Mtendaji Mkuu, Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC). Kabla ya uteuzi huo Erio alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Pia Rais Samia amemteua Dk. John Kedi Mduma kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF). Kabla ya uteuzi huo Dkt Mduma alikuwa Afisa Mtendaji Mkuu, Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uteuzi wa Makatibu Tawala ulianza jana, na wataapishwa Jumatano asubuhi katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoa.

HABARI KITAIFA

# Vikwazo biashara 30 Kenya, Tanzania vyaondolewa

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema vikwazo vya kibiashara 30 kati ya 64 vilivyokuwa vinaikabili Tanzania na Kenya vimetatuliwa.

Alisema: "Jumla ya masuala 64 yamejadiliwa na kati ya hayo masuala 30 yametatuliwa, masuala mengine 34 yaliobaki yamewekewa mkakati maalum na muda wa utekelezaji."

Alisema katika mkutano wa tano wamejadili masuala mbalimbali ya biashara katika sekta za kilimo, forodha, uhamiaji na usafirishaji.

Alisema miongoni mwa masuala waliyoyatatua kwa upande wa Tanzania ni pamoja na kuwezesha upitishaji wa bidhaa mpakani, hususani vinywaji baridi kama vile juisi kutoka Tanzania kwenda Kenya.

Lingine ni kuondolewa kwa tozo za ukaguzi zilizokuwa zinatozwa na mamlaka za Kenya kwenye bidhaa za Tanzania, ikiwamo unga wa ngano, zenye alama ya ubora kutoka mamlaka husika Tanzania.

"Kuwezesha upitishaji wa mahindi kutoka Tanzania kwenda Kenya, kuondoa ushuru wa asilimia 25 kwenye bidhaa za kioo kutoka Tanzania kwenda Kenya,"alisema.

Alisema kwa upande wa Kenya masuala ambayo wamekubaliana ni kutoa upendeleo kwa bidhaa za saruji zinazozalishwa nchini humo ambazo zinakidhi matakwa ya vigezo vya uasili wa bidhaa vya na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lingine ni kutoa upendeleo maalum kwa vinywaji kutoka Kenya ikiwamo juisi za nanasi baada ya kukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kuhakikisha bidhaa zinazoharibika haraka kama vile maziwa zinapewa kipaumbele zinapovuka mpaka kutoka Kenya kuingia Tanzania kwa kuzingatia taratibu za sheria ya forodha.

"Kuongeza muda wa kibali cha kuingiza bidhaa za mifugo kutoka siku 15 hadi siku 30," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema katika hatua nyingine wameazimia kudumisha ushirikiano kuhusu uchumi, biashara na uwekezaji.

Prof. Mkumbo alisema hiyo ni pamoja na kufuata taratibu zote walizokubaliana kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi zetu mbili ni wanachama.

Pia wamekubaliana kuunda timu ya maofisa wanne, maofisa wawili kutoka kila nchi, kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya mkutano huu, kuhakikisha kuwa vikwazo vilivyotatuliwa havijitokezi tena.

Waziri wa Biashara na Viwanda wa Kenya, Betty Maina, alisema wamekubaliana makubaliano hayo 30 lakini baada ya miezi mitatu makubaliano 34 yaliyobaki yatakua yamepatiwa ufumbuzi.

# Mwinyi aeleza alivyoruhusu shule binafsi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema uamuzi wa kuruhusu uwekezaji binafsi na kuanzisha shule za kulipia wakati wa utawala wake, ulilenga kupunguza mzigo kwa serikali.

Katika kitabu chake kiitwacho 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mzee Mwinyi anaeleza kwamba shule hizo hususani sekondari za umma idadi yake iliongezeka kidogo, hivyo za binafsi ziliisaidia serikali kupanua wigo wa utoaji elimu hiyo.

"Mojawapo ya mambo yaliyoniuma sana ...ni sharti tulipewa na mashirika ya fedha ya kimataifa kwamba tupunguze matumizi kwenye huduma za jamii na kuwataka wananchi wachangie ili kufidia upungufu." anaeleza Mzee Mwinyi kwenye kitabi hicho.

"Mojawapo ya maamuzi tuliyoyafanya ilikuwa kuruhusu taasisi za dini na wawekezaji binafsi kuanzisha shule za kulipia ili kupunguza mzigo kwenye shule za serikali," anasema Mzee Mwinyi.

"Katika kuweka mkazo kwenye elimu ya msingi kwa wote, elimu ya sekondari haikupanuka sana wakati wa Mwalimu Nyerere. Miaka 10 kabla sijaingia madarakani kulikuwa na shule za sekondari za umma 84 mwaka 1977 zikafikia hadi 86, mwaka 1986."

Anasema wakati wa uongozi wake, asilimia tatu pekee ya watoto wenye umri wa miaka 14 hadi 17, walikuwa wanasoma shule za sekondari.

Mzee Mwinyi anasema uchumi kuwa duni pamoja na wahisani kujitoa katika kutoa msaada na kwamba mapato ya nchi hayakuwezesha kuhudumia ipasavyo mtandao mpana wa elimu.

Anabainisha kwamba: "Ikabidi tuanze kuchangisha wazazi, tukapunguza sana ajira mpya ikiwamo walimu...ujenzi wa shule mpya ukasimama na hata ukarabati wa zilizokuwepo nao ukakwama."

**"Mojawapo ya maamuzi tuliyoyafanya ilikuwa kuruhusu taasisi za dini na wawekezaji binafsi kuanzisha shule za kulipia ili kupunguza mzigo kwenye shule za serikali,"**





NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street

P. O. Box 6707, Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045, Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

## NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa deni kwa hiari muda huo ukifika bila kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA,** Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, mnada utafanyika kuanzia saa 04:30 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA .**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | AVCC TRADERS | Hati Na. 100466, Kiwanja No.2016, Kitalu "B" Mbweni, Dar es Salaam City. Ukubwa wa eneo sqm 10959. | 19/06/2021 kuanzia saa 04:30 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. **Kwa mawasiliano zaidi piga simu No: 0782 065 914 / 0712 073 680**

# Bei mafuta kula yauma, yapuliza

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya mafuta ya kula bado haikamatiki katika baadhi ya maeneo nchini licha ya bidhaa hiyo kuwapo kwa wingi madukani.

Kutoshuka bei kwa bidhaa hiyo kumesababisha baadhi ya wananchi kutumia mbadala kwa kuweka karanga kwenye mboga.

Uchunguzi wa Nipashe katika baadhi ya maduka yanayouza bidhaa hiyo, umebaini bei katika baadhi ya mikoa imeendelea kuwa juu, licha ya serikali kufanya jitihada za kuleta shehena kubwa ya bidhaa hiyo.

Hivi karibuni bungeni, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara yake, alisema serikali inakuja na mkakati wa kukabiliana na uhaba pamoja na kupanda bei kwa mafuta ya kula nchini kwa kutumia mbegu mpya za alizeti pamoja na kuhamasisha kilimo cha michikichi.

Waziri Mkenda alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza uhaba wa mafuta unaosababisha kupanda bei kwa bidhaa hiyo na kubaki kuwa historia nchini.

Alisema katika kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula, wizara itaendelea kueneza mbinu ya kilimo cha mkataba iliyoanza kutumiwa na baadhi ya wenye viwanda kama vile Pyxus ili kuchochea uzalishaji na uhakika wa soko kwa mkulima. Pia, alisema katika mwaka 2021/2022 wizara itahamasisha uzalishaji wa chikichi kufikia tani 50,000 na alizeti kufikia tani 1,000,000.

**HALI ILIVYO SASA**

**TANGA**

Uchunguzi wa Nipashe katika maduka mbalimbali mkoani hapa umebaini mafuta hayo yakiuzwa bei ya juu na baadhi ya maduka yakiadimika.

Wafanyabiashara wa maduka ya reja reja, Ally Omar na Karim Magwila, katika barabara ya 15 walisema bei ya bidhaa hiyo inaendelea kupaa kutokana na kuadimika kwa wafanyabiashara wakubwa wanaoagiza bidhaa hiyo.

"Bei hizi zinatokana na kuadimika kwa wafanyabiashara wakubwa, kiukweli hata faida yake ni ndogo sana," alisema Omari.

Alisema ujazo wa lita moja kwa sasa yanauzwa kwa Sh. 5,000 huku katoni yenye lita 12 ikiuzwa Sh. 54,000, wakati awali lita moja ilikuwa ni Sh. 3000 hadi Sh. 3,500.

Ujazo wa lita tatu yanauzwa kwa Sh. 15,000 na katoni yenye chupa sita huuzwa Sh. 86,500, ndoo yenye ujazo wa lita 10 inauzwa Sh. 43,500 kwa rejareja na jumla ni Sh. 42,800.

Mafuta ya alizeti lita moja ni Sh. 7,500 huku katoni yenye chupa 12 ikiuzwa Sh.78,000, ujazo wa lita tatu ikiuzwa Sh. 20,000 kwa lita moja na Sh. 109,000 kwa katoni ya chupa sita.

**KILIMANJARO**

Wafanyabiashara ndogo katika soko la Lawate, wilayani Siha, walisema bei haijashuka.

Walisema awali mafuta ya kula ya ujazo wa lita tatu aina ya Sunola yaliuzwa kwa Sh. 16,000 na sasa yanauzwa kwa Sh. 24,000 huku lita tano iliyokuwa ikiuzwa Sh. 20,000 inauzwa Sh. 32,000 hadi Sh. 34,000.

Mfanyabiashara Erick Mlay, alisema kwa sasa lita moja ya mafuta inauzwa 6,000, lita tatu ni Sh. 18,000 na lita tano kwa Sh. 35,000.

**SHINYANGA**

Katika baadhi ya maduka mkoani hapa bei imeendelea kuwa juu kwa miezi minne iliyopita na kufanya gharama za maisha kupanda.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko kuu mkoani humo alisema bei ya mafuta haijashuka.

Alisema kuanzia Januari mwaka huu, lita moja ya mafuta ya kula ilikuwa ikiuzwa Sh. 4,000, lakini sasa inauzwa Sh. 5,000, lita tano inauzwa Sh. 25,000 awali ilikuwa Sh. 23,000.

Alisema lita 20 inauzwa Sh. 85,000, wakati mwezi Januari ilikuwa yakiuzwa Sh. 77,000.

Katika Wilaya ya Kahamabei lita 20 yanauzwa Sh. 85,000 bei ya awali ilikuwa Sh. 83,000. Mafuta ya kula lita 10 kwa sasa yanauzwa Sh. 45,000, awali yalikuwa yanauzwa Sh. 23,000.

**MWANZA**

Bei inazidi kupaa, ndoo ya lita 20 inauzwa Sh. 83,000 badala ya Sh. 58,000 ilivyokuwa miezi miwili iliyopita.

Mfanyabiashara Mohammed Kassimu, aliiambia Nipashe mafuta ya lita tano yalikuwa yakiuzwa Sh. 20,000, sasa ni Sh. 27,000.

Lita tatu yaliyokuwa Sh. 12,000 sasa ni Sh. 16,000 na lita moja ya alzeti inauzwa Sh. 7000 badala ya Sh. 6000, lita moja ya mafuta ya Korie yanauzwa Sh. 5,000 badala ya Sh. 4500.

**KAGERA**

Mjini Bukoba mafuta ya alizeti ya ujazo wa lita tano yanauzwa Sh. 30,000 badala ya Sh. 17000, mwanzoni mwa mwaka huu.

Aidha, lita 20 yanauzwa Sh. 115,000 badala ya Sh. 85,000 na mafuta aina ya Mkwano lita tano yanauzwa Sh. 26000 badala ya Sh. 18,000 na ujazo wa lita 20 yanauzwa Sh. 104,000 badala ya Sh. 90,000.

**DODOMA**

Katika Jiji la Dodoma kuna afueni baada ya kushuka kutoka Sh. 7,000 kwa lita moja ya mafuta ya alizeti hadi Sh. 5,000.

Mmoja wa wasindakaji wa mafuta ya alizeti jijini humo, Selina Kuziganika, alisema kupungua kwa bei hizo kunachangiwa na kuanza kwa msimu wa mavuno ya alizeti.

Kuziganika, alisema msimu wa mavuno hivi sasa umechangia ungozeko la uzalishaji ambao hapo awali ulishuka kutokana na kukosekana kwa malighafi hiyo.

Hata hivyo, bei hiyo imetofautiana kutokana na ubora wa mafuta, katika maduka yaliyotembelewa.

Sandrop, yanauzwa kwa Sh. 38,000 kwa ujazo wa lita tano.

**MBEYA**

Bei imeshuka kutoka Sh. 130,000 na 140,000 kwa lita 20 mwezi Aprili, mwaka huu hadi Sh. 100,000 na 120,000, mwezi huu (Mei), kutokana na ongezeko la alizeti.

Wafanyabiashara wa bidhaa hiyo walisema bei hiyo imeshuka kutokana na mavuno ya alizeti katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuongezeka.

Mmoja wa wajasiriamali wa mafuta katika eneo la Sokoine jijini hapa, Subira Mwakyoma, alisema mwezi Aprili lita moja waliuza kati ya Sh. 7,000 na 7,500 na sasa imeshuka na kufikia kati ya Sh. 5,000 na 6,000.

Hata hivyo, alisema miaka ya nyuma miezi kama hii ya mavuno mafuta yalikuwa yakiuzwa Sh. 60,000 kwa lita 20 na lita moja Sh. 3,000.

"Kwa sasa ukienda kwenye mashine tunanunua Sh. 100,000 na tukija huku mtaani tunauza kwa bei tofauti, binafsi nauza lita moja Sh. 6,000 kwa hiyo dumu moja napata faida Sh. 20,000 na wapo wanaouza Sh. 5,000 na faida yao ni Sh. 15,000," alisema Subira.

Aidha, mafuta aina ya alizeti lita tano yanauzwa Sh.25,000 na lita moja Sh.5,500, huku Sundrop lita tatu yakiuzwa Sh.23,000.

**MANYARA**

Wauzaji wa mafuta ya alizeti mkoani Manyara walisema bei imeanza kushuka kutokana na wakulima wa zao hilo kuanza kuvuna.

Mkamuaji wa mafuta, Africans Panga, alisema wanauza dumu la lita 20 kwa Sh. 70,000 na dumu la lita tano kwa Sh. 20,000. Awali dumu la lita tano liliuzwa Sh. 27,000 na lita 20 kwa Sh. 110,000.

Naye Bakari Khatibu muuzaji wa mafuta kwa rejareja alisema bei imeshuka kwa sababu wakulima wameanza mavuno. Alisema anauza lita tano kwa Sh. 22,000 na lita 20 kwa Sh. 75,000.

**ARUSHA**

Maduka kadhaa jijini Arusha yaliyotembelewa na Nipashe yalikutwa yakiuza mafuta ya kula bei juu kwa zaidi ya miezi mitano sasa.

Katika baadhi ya maduka mafuta aina ya safi ya ujazo wa lita 10 yaliuzwa Sh. 38,000 mwezi Julai mwaka jana na lita 20 yaliuzwa Sh. 77,000.

Kwa sasa lita 20 yanauzwa Sh. 88,000 kwa bei ya jumla na rejareja Sh. 89,000, huku yenye ujazo wa lita 10 yakiuzwa Sh. 45,000 kwa rejareja, bei ya jumla Sh. 44,000.

Mafuta ya Sundrop lita tatu yanauzwa Sh. 18,000 hadi 20,000 na alizeti lita tano yanauzwa Sh. 20,000.

**●Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi, Tumaini Mafie (ARUSHA), Jaliwason Jasson (Manyara), Boniface Gideon na Lulu George (Tanga), Angela Mhando na Mary Mosha (Kilimanjaro). Marco Maduhu, Shinyanga, Shabani Njia (Kahama), Neema Emmanuel (Mwanza), Restuta Damian (Bukoba), Paul Mabeja, Salome Kitomari (Dodoma) na Nebart Msokwa (Mbeya).**


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**CHARLES SIMONI NG'ENG'ELE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA COASTER** yenye namba za usajili **T 259 CYV Chassis No. HZB400005647,** Engine **No.1HZEAA5647.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/R-B/271151/2021.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**MARIA CHARLES SHIJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1845-0020** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SEEKE SEKONDARI** mwaka **2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/248986/2021.**

**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA SIKU 14/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA CRDB** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili.Vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MKOPAJI/MMILIKI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA KUANZIA |
|---|---|---|---|---|
| ALOYCE PACAL JAVA | Nyumba | Mivumoni,Umoja road mtaa wa Kisiwani-Dar es salaam | 19.6.2021 | Saa 4:00 asubuhi |
| MOHAMED RASHID MOHAMED | Nyumba ya kulala wageni yenye CT. Na 3309-MTW,L.O Na. 296157 | Mbovu-Masasi mjini | 19.6.2021 | Saa 4:00 asubuhi |
| MBARAKA MUSA CHIHANGO | Nyumba yenye CT. Na 6709-MTW,L.O Na. 296592 | Jida-Masasi | 19.6.2021 | Saa 6:00 mchana |
| BEATUS ALPHONCE KISUSI | Nyumba | Kishiri B-Mwanza | 19.6.2021 | Saa 4:00 asubuhi |
| HAMISI HASHIMU MKOPITI | Nyumba yenye CT. Na 6367-MTW,L.O Na. 256055 | Ujenzi-Newala | 23.6.2021 | Saa 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0713 295747, 0746 422519**

Victoria Finance

**Victoria Finance Plc**
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DAVID NASONGELYA | GARI | TOYOTA RUNX T 516 DHR | UMOJA PROFESSINALS | 14-06-2021 |
| 2 | ZACHARIA G. LYIMO | GARI | FORD RANGER T 572 CVC | UMOJA PROFESSINALS | 14-06-2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Taratibu na gharama za kubadili hati miliki kadi ya gari ni juu ya mnunuzi.

TANGAZO


GO
na
NMB
Usiachwe
@GOnaNMB
0747 333 444
*Vigezo na Masharti Kuzingatiwa
Scan GO QR :
nmbbank.co.tz/GO

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zitafute wadhamini, zisibweteke na huu wa TFF

**MSIMU** wa 2020/21 wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaelekea ukingoni kwani ukiondoa baadhi ya timu ambazo zina viporo, nyingi zimebakisha raundi nne tu kuhitimisha mchakamchaka wa michezo 34 inayopaswa kuchezwa kwa kila timu msimu huu.

Kwa ujumla mbio za ubingwa sasa zinaelekea kuachiwa farasi mmoja, kutokana na mabingwa watetezi, Simba kuwa kileleni mwa msimamo wakiwa na pointi 64 na viporo vitatu huku Yanga inayoshika nafasi ya pili ikiwa na alama 61 zilizotokana na michezo 29.

Hata hivyo, kunaonekana kutakuwa na vita kali ya kuwania kumaliza nafasi ya pili kutokana na Azam FC iliyoshuka dimbani mara 30, kuifukuzia Yanga kwa karibu baada ya kujikusanyia alama 60 hadi sasa. Ushindani huo wa nafasi ya pili, unachagizwa hasa na kufanya vizuri kwa Simba kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, hivyo kuiongezea Tanzania pointi na kuwa kati ya nchi 12 zitakazotoa wawakilishi wanne kwenye michuano ya kimataifa; timu mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Na kama ilivyo kwa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), bingwa wa Ligi Kuu na mshindi wa pili ndizo timu zitakazopata nafasi ya kuiwakilisha nchi Ligi ya Mabingwa Afrika huku mshindi wa Kombe la FA na atakayeshika nafasi ya tatu Ligi Kuu Bara, zikiangukia Kombe la Shirikisho. Hivyo, nafasi hizo ndizo zinazoongeza ushindani kwenye Ligi Kuu, lakini vita vingine vipo kwenye timu nne zinazopigana vikumbo mkiani kukwepa kushuka daraja ili kuendelea kukipiga kwenye ligi hiyo ambayo tayari TFF imeiongezea thamani kutokana na kuongezeka kwa dau la mdhamini wa kurusha matangazo ya televisheni.

Ni wazi kila timu inatamani kucheza Ligi Kuu msimu ujao kutokana na kuongezeka kwa thamani ambayo inakwenda kuzipunguzia mzigo wa mishahara baada ya TFF kusaini mkataba mnono wa miaka 10 wenyewe thamani Sh. bilioni 225.6 na Azam Media Limited wa kuendelea kurusha matangazo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia msimu wa 2021/22 hadi 2030/31.

Ni wazi wanufaika wakubwa wa mkataba huo ni klabu za Ligi Kuu na moja ya masharti ya TFF kwa klabu ni kuhakikisha kiasi kitakachogawiwa kila mwezi kwa kwa klabu ni kuhakikisha kinaelekezwa kwenye mishahara ya wachezaji, jambo ambalo lilikuwa likizisumbua klabu nyingi katika kuwalipa wachezaji wao.

Si hilo tu, pia msimu ujao ambao utashirikisha timu 16, kuanzia bingwa ambaye ataibuka na bonasi ya Sh. milioni 500, mshindi wa pili Sh. milioni 250, wa watatu milioni 225 na mshindi wa nne akiibuka na Sh. milioni 200, bonasi hizo zitaendelea kushuka hadi timu itakayoangukia kucheza mechi ya mchujo 'Play off', ambayo italamba milioni 25, hivyo ni utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu kuwahi kutokea nchini.

Nipashe hatuna budi kuipongeza TFF na Azam Media Limited kwa kufanikisha udhamini huo, ambao tunaamini utakwenda kuongeza ushindani mkubwa kwenye ligi yetu kuanzia msimu ujao, hivyo kuzidi kuwa bora zaidi kutoka nafasi ya nane ambayo inashika barani Afrika. Lakini pamoja na juhudi hizo za TFF, huu si wakati wa klabu ambazo zitabaki Ligi Kuu, zilizopanda na zile zitakazopanda kubweteka na fedha hizo za mdhamini wa ligi kwa upande wa urushaji wa matangazo.

Tunatambua uendeshaji wa klabu za soka ni gharama kubwa sana, hivyo kiasi hicho kitakachotolewa na TFF kupitia udhamini wa Azam Media Limited pamoja na mdhamini mkuu, Kampuni ya Vodacom na wadhamini wenza wengine wa ligi hiyo, bado hakiwezi kutosha kwa uendeshaji wa klabu. Hivyo, huu sasa ni wakati kwa kila klabu kuanza kuingia sokoni kujitafutia wadhamini wao wengine, mfano mdhamini wa jezi na vifaa vyote vya michezo ili kujiongezea kipato na kuepuka kutegemea udhamini huo wa TFF na Azam Media Limited na pamoja na mapato ya mlangoni ambayo siku hizi yameshuka sana. Tunaamini kwa kufanya hivyo, kutazifanya klabu kuwa na utajiri mkubwa wa kipato, hivyo kuongeza ushindani kwenye ligi na soka la Tanzania kuzidi kukua kila uchao, jambo ambalo litawavutia wawekezaji wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Karia anastahili kongole ushauri matumizi fedha za udhamini TFF

Na Adam Fungamwango

**KUMEZUKA** mjadala mkali juu ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuzishauri klabu jinsi ya kutumia pesa zitakazotolewa kutoka Kampuni ya Azam Media kutokana uhamini wa matangazo ya televisheni kwenye Ligi Kuu Bara.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alizishauri klabu kutumia pesa hizo kwenye mishahara, usafiri na matibabu ya wachezaji. Hii ni baada ya kuingia mkataba wa miaka 10 na Kampuni hiyo ya Azam Media Limited kuanzia msimu ujao wa ligi. Jumla ya Sh. bilioni 225.6 zitatolewa kwa miaka hiyo kwa ajili ya mechi kuonyeshwa laivu kwenye luninga. Katika hafla hiyo ya utiaji saini, Rais Karia alizishauri klabu jinsi ya kuzitumia pesa hizo, hasa kwenye sehemu za msingi.

Hata hivyo, ushauri huo umeonekana kupokewa vibaya na baadhi ya wachambuzi na wadau wa michezo kwenye mitandao ya kijamii wakidai kuwa TFF haina haki ya kuzipangia klabu matumizi.

Wakadai kuwa klabu hizo zimeuza haki zao ya kuonyeshwa kwenye televisheni, hivyo zina haki ya kutumia pesa zinavyotaka kwa sababu si za misaada.

Wakatoa mfano wa mtu anayeuza gari, mnunuzi hawezi kumpa pesa na kumpangia kuwa anunue nyumba na asinunue gari lingine ama asiende kunywea pombe au kuoa mke mwingine. Ni sawa mtu yeyote anayeuza kitu chake hapangiwi matumizi ya pesa.

Hata hivyo, kwa ndugu wa karibu ambaye anamfahamu jinsi ndugu yake anavyopata tabu anapokuwa hana pesa, anaweza kumshauri nini afanye atakapoona amefanikiwa kuzipata. Ni kwa sababu ukosefu wa pesa wa ndugu yake humuathiri hata yeye.

Mfano kuna mtu ambaye akiwa hana pesa anasumbua sana ndugu zake. Hawana raha, kila siku kupiga 'mizinga' na kwenda kuvizia chakula. Ndugu humsaidia kwa kadri ya uwezo wao.

Siku wakiona amepata pesa, wana uwezo wa kumshauri nini cha kufanya, nini cha kununua, nini ajiepushe nacho ili pesa zile zimsaidie na wao wasilazimike tena kusumbuliwa.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Rais Karia, kuamua kushauri kuwa pesa zitumike zaidi kwenye mishahara ya wachezaji, usafiri na matibabu, hivyo yupo sahihi kabisa. Mara kadhaa tumeona wachezaji wengi wakilalamika kutolipwa mishahara hadi ya miezi minne na wakidai kuishi kwa posho tu.

Tumeshawahi kuona timu zikisafiri kwa shida kwenda kwenye vituo vya mechi kiasi cha kutishia hata timu pinzani kupata ushindi wa bure. Pia msimu wa mwaka juzi na mwaka jana, tulizisikia baadhi ya klabu zikitishia kutoendelea na Ligi Kuu kutokana na ukata.

Kuna taarifa za ndani kuwa TFF iliingilia kati na kuzikopesha pesa ili ziendelee kuwapo kwenye Ligi Kuu kwa sababu kama zingejiondoa si tu kwamba zingevuruga utaratibu wote wa ligi, timu zilizocheza nazo kufutiwa matokeo, lakini pia ingekuwa ni doa kwa Shirikisho na Tanzania kwa ujumla kuwa na ligi ambayo timu zinajiondoa kwa ukata.

Baadhi ya wachezaji wamekuwa wakiugua au kupata majereha, lakini klabu zao zimeonekana kushindwa kuwatibia. Matokeo yake wamekuwa wakijiuguza wenyewe kwa msaada wa mashabiki, ndugu na marafiki zao.

Klabu zingine ni mpaka taarifa zitoke kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ndipo huona aibu na kuanza kuwatibia. Haya yote TFF wanayaona. Ndiyo maana wameshauri au kuelekeza hivyo.

Lakini hebu tujiulize. Kama klabu itapokea pesa hizo za udhamini halafu viongozi wake wakaanza kuzitumia nje ya mishahara, matibabu, usafiri, kambi na chakula cha wachezaji, kisa tu zisipangiane matumizi, hivi wanafaa kweli kuwa viongozi wa soka?

Ni kweli inawezekana kuna matumizi mengi, lakini aliyosema Karia ndiyo mama ya pesa za kwenye soka. Hapa pesa hizi zinaonekana kama ni nyingi sana, lakini huko mbele tunaweza kusikia kuna timu zinalalamika ukata pia. Hii ni kwa sababu ya kutumiwa vibaya. Lakini kwenye masuala ya mpira bado hazitoshi pia. Timu pia zina wajibu wa kutafuta wadhamini wao.

Ndiyo maana Karia amezishauri. Isije ikatokea baadhi ya viongozi wakazitumia vibaya, wakawapa shida wachezaji wao na ushiriki wao wa ligi ukawa wa kusuasua.

Halafu inawekana kabisa lawama zikarudi tena kwa TFF ambayo kwa sasa ndiyo imekuwa kimbilio la baadhi ya wanamichezo kujifichia, kwa hilo ninasema kongole Karia kwa ushauri makini na wenye tija kwa maendeleo ya soka letu.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

**28/05/2021**

# TANGAZO LA ZABUNI MBALIMBALI ZA MWAKA 2021/2022

(1).Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inatangazia Kampuni , taasisi, vikundi, wafanya biashara au watu binafsi wenye uwezo wa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmasahauri, kufanya ufundi wa kazi za majengo, kazi za miundombinu ya Umeme, kupanga vibanda vya Halmashauri au maeneo ya kujenga vibanda vya biashara au kutoa bidhaa maalum/huduma kuanzia tarehe 01/07/2021 hadi tarehe 30/6/2022 kama ilivyoainishwa katika makundi A-H hapa chini:-

**(A) ZABUNI ZA UWAKALA MBALIMBALI- MAZAO YA MISITU, KILIMO NA MAEGESHO**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 1 | Zabuni ya Ushuru wa mazao ya misitu |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 2 | Zabuni ya Ushuru wa mazao ya Kilimo tofauti na Korosho |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 3 | Zabuni ya Ushuru wa mabasi makubwa stendi ya Kichemchem Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 4 | Zabuni ya Ushuru wa maegesho ya Kastamu Ufukweni Bagamoyo |

**(B) ZABUNI ZA WAKALA MBALIMBALI – VYOO NA DAMPO**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 1 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Kastam (TRA ya zamani) |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 2 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Soko jipya |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 3 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha soko la MIVARF |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 4 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Stendi ya Mabasi makubwa Kichemchem Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 5 | Zabuni ya Ushuru wa choo cha Stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 6 | Zabuni ya Ushuru wa Dampo la taka ngumu Bagamoyo |

**(C) ZABUNI YA UPANGAJI KWENYE MAJENGO NA VIBANDA VYA BIASHARA**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 1 | Zabuni ya upangaji wa karakana ya magari na maegesho yake |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 2 | Zabuni ya upangaji kwenye mgahawa wa Halmashauri uliopo kwenye stendi ya mabasi madogo Dunda Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 3 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 28 kilichopo soko jipya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 4 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 32 kilichopo soko jipya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 5 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 35 kilichopo soko jipya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 6 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 36 kilichopo soko jipya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 7 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 59 kilichopo soko jipya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/03- LOT 8 | Zabuni ya upangaji kwenye kibanda Na 60 kilichopo soko jipya Bagamoyo |

**(D) ZABUNI YA KUWACHUJA MAFUNDI WA KAZI NDOGONDOGO ZA KIFUNDI**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/W/PRE/01-LOT I | Zabuni ya kuwachuja Mafundi wa kazi ndogondogo za Ujenzi na ukarabati wa majengo na ofisi katika Kata, shule mbalimbali, Hospitali, vituo vya afya na zahanati. |
| LGA/014/2021/2022/W/PRE/01-LOT 2 | Zabuni ya kuwachuja mafundi wa kazi ndogondogo za miundo mbinu ya maji katika Halmashauri, kata, shule mbalimbali, vituo vya afya na zahanati |
| LGA/014/2021/2022/W/PRE/01-LOT 3 | Zabuni ya kuwachuja mafundi wa kazi ndogon za miundo mbinu ya umeme |
| LGA/014/2021/2022/W/PRE/01-LOT 4 | Zabuni ya kuwachuja mafundi wa kazi ndogondogo za miundombinu ya TEHAMA |
| LGA/014/2021/2022/W/PRE/01-LOT 5 | Zabuni ya kuwachuja mafundi wa kazi ndogondogo za matengenezo na ukarabati wa meza, viti na madawati katika shule mbalimbali. |

**(E) UTOAJI WA BIDHAA MAALUM**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/G/PRE/01-LOT 1 | Zabuni ya kutoa chaki katika shule zote za Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo |
| LGA/014/2021/2022/G/PRE/01-LOT 2 | Zabuni ya kutoa gesi kwa ajili ya kukaangia samaki katika soko la kisasa la Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo |

**(F) UTOAJI WA HUDUMA YA UCHAPISHAJI, KUDURUFU NYARAKA MBALIMBALI NA/AU KUANDIKA NAMBA ZA UTAMBULISHO KWENYE MALI ZA KUDUMU**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/N/PRE/01 | Zabuni ya utoaji wa huduma za uchapishaji na kudurufu nyaraka mbalimbali |
| LGA/014/2021/2022/N/PRE/02 | Zabuni ya uandishi wa namba za utambulisho kwenye mali za kudumu kwenye ofisi za Halmashauri, shule, Hospitali, vituo vya afya na zahanati. |

**(G) ZABUNI YA UTOAJI WA HUDUMA YA MATENGENEZO MADOGO YA MAGARI, PIKIPIKI, MITAMBO, VYOMBO VYA MAJINI NA VIFAA TIBA**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/N/PRE/03 | Zabuni ya matengenezo madogo ya magari, pikipiki. Mitambo na vyombo vya majini . |
| LGA/014/2021/2022/N/PRE/04 | Zabuni ya matengenezo ya vifaa tiba kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati |

**(H) ZABUNI YA KUPANGA ENEO LA KUJENGA KIBANDA CHA BIASHARA KWENYE STENDI YA MABASI KICHEMCHEM BAGAMOYO**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| **LGA/014/2021/2022/HQ/N/04-LOT 01- 04** | **Zabuni ya kupanga eneo la kujenga vibanda vya biashara ukubwa wa 2.5mx3m kwenye stendi ya mabasi kichemchem Bagamoyo** |
| **LGA/014/2021/2022/HQ/N/04-LOT 05-12** | **Zabuni ya kupanga eneo la kujenga vibanda vya Mama/Baba lishe vyenye ukubwa wa 3mx5m kwenye stendi ya mabasi kichemchem Bagamoyo** |

**(2) MASHARTI KWA WAOMBAJI WA ZABUNI HIZI**

1. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo
2. Mwombaji wa zabuni katika kundi **A, D, E, F na G** alipe ada ya maombi ya zabuni ya **Tshs. 50,000/=** kwa kila zabuni; fedha hizo hazitarudishwa.
3. Mwombaji wa zabuni katika kundi **B, C na H** alipe ada ya maombi ya zabuni ya **Tshs. 20,000/=** kwa kila zabuni; fedha hizo hazitarudishwa.
4. Mwombaji wa zabuni **E, F au G** awe na Leseni hai ya biashara husika pamoja na **TIN/VAT**
5. Aidha mwombaji wa zabuni **E, F au G** awe na Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni pamoja na M**emorandum and Articles of association/Extract from the Register** ili wamiliki wajulikane.
6. Mwombaji ambaye ni kampuni, taasisi au kikundi aambatanishe hati maalum ya kisheria **( Special Power of Attorney)** kwa ajili ya mtia saini wake.
7. Mwombaji wa uwakala wa kukusanya mapato ya Halmashauri aambatanishe Bank statement za miezi mitatu ya **Februari, Machi na April 2021.**
8. Maombi yaambatane na tamko la **dhamana ya Zabuni (Bid Securing declaration).**
9. Dhamana ya utendaji **"Performance Bond"** ya 10% ya thamani ya mkataba kwa mwezi mmoja ilipwe na wakala kabla ya kusaini mkataba kwa wakala atakayeshinda.
10. Wakala atakayeshinda atatakiwa kuilipa Halmashauri mapato ya mkataba ndani ya siku tano za mwanzo wa kila mwezi.
11. Mwombaji ataje eneo anakotoka au ofisi za kampuni/Taasisi zilipo au kikundi kilipo (physical address) pamoja na kutoa namba za simu na/au barua pepe kwa ajili ya mawasiliano.

(3). **Vitabu vya Zabuni** na maelezo mengine vinapatikana Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni , **S.L.P. 59, Bagamoyo,** kuanzia Saa **2.30** asubuhi mpaka **Saa 9.30 alasiri (Jumatatu – Ijumaa).**

(4). Nyaraka za maombi ziwe ni nakala **moja halisi** pamoja na nakala **ya kawaida moja, zote** zifungwe kwa **LAKIRI,** juu ya bahasha iandikwe **"NAMBA NA JINA LA ZABUNI INAYOOMBWA"**na zitumbukizwe katika sanduku la zabuni lililoko Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo baada ya kupokelewa na kusajiliwa kwenye ofisi ya katibu wa zabuni. Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Katibu**
**BODI YA ZABUNI HALMASHAURI YA WILAYA**
**S.L.P 59, BAGAMOYO**

(5). Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 15/06/2021 saa 5.00 asubuhi. Zabuni zote zitafunguliwa muda mfupi baada ya muda huo katika ukumbi wa mikutano Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Waombaji wote wanakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zao.

**Fatuma O. Latu**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**BAGAMOYO**



Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Advent Tweve akizungumza mbele ya wananchi wa kata ya Sinde wakati wa kutambulisha zaoezi la kutambua kila kipande cha ardhi katika kata hiyo hilo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wawekezaji waomba udhibiti uvamizi Ranchi za Taifa

**Na Mbaraka Kambona**

WAWEKEZAJI wa muda mrefu katika vitalu vya Ranchi za Taifa wameiomba serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti uvamizi unaofanywa na baadhi ya wananchi katika maeneo hayo kwa kuwa umekuwa kikwazo katika kuendeleza sekta ya mifugo nchini.

Walitoa ombi hilo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alipokutana nao katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO), kilichofanyika jijini Dodoma juzi.

Wakieleza changamoto wanazozipata katika uwekezaji wao walisema kuwa pamoja na mambo mengine, suala la wananchi kuvamia maeneo yao waliyowekeza linakwamisha kufanya shughuli zao za kuendeleza ufugaji wa kisasa.

Mwenyekiti wa wawekezaji hao, Jackson Mwasonga, alisema wavamizi wanakwamisha shughuli zao na kuna wakati wanalazimika kutoa hela kwa wavamizi hao ili waweze kuchunga mifugo yao katika maeneo wanayomiliki kihalali. "Mheshimiwa waziri inafika wakati tunatoa hela ili tuweze kuchunga na kunusuru mifugo yetu, uvamizi unatishia maisha yetu na mali zetu, tunaomba mtangaze wavamizi waondoke ili tuweze kufanya ufugaji unaohitajika kwa amani," alisema Mwasonga.

Projestus Gamasho, Mwekezaji katika Ranchi ya Kitengule, mkoani Kagera alisema ranchi hiyo kwa sasa imevamiwa na tembo zaidi ya 600 na kuharibu miundombinu yote huku akiiomba serikali kutoa msaada wa haraka kuwaondoa tembo hao.

Mwekezaji wa Ranchi ya Uvinza, Kigoma, Benard Katamba, alisema wavamizi katika Ranchi hiyo sio tu wamechukua maeneo yao, pia wanaiba mifugo yao kila wakati jambo linalowakatisha tamaa ya kuendelea na ufugaji.

"Sisi Wawekezaji wa Ranchi ya Uvinza tumevamiwa hasa, mpaka sasa nimeshaibiwa ng'ombe 25 na mbuzi 150 na sina matumaini yoyote ya kuwapata, kwa kweli tunaomba msaada wa serikali," alisema Katamba.

Mwekezaji katika Ranchi ya Misenyi, mkoani Kagera, Nestory Lugakingira, akitoa ushauri kwa serikali alisema kuwa ili waweze kuishi kwa amani serikali ione uwezekano katika yale maeneo yaliyovamiwa yagawiwe kwa wavamizi hao na sehemu itakayobaki waitumie kuendeleza mifugo yao na kuepuka migogoro na wananchi hao.

Akitoa ufafanuzi wa hoja za wawekezaji hao, Waziri Ndaki alisema serikali ipo pamoja na wawekezaji hao na itachukua hatua kali kwa wote wanaovamia maeneo ya Ranchi kinyume na sheria.

"Ninaelewa kwamba kuna maeneo ambayo wananchi wanakaa na kuwaondoa itakuwa ni uvunjifu wa haki za binadamu, maeneo hayo tutayainisha na ili tuone kama tunataka kuendelea nayo au tukubali maeneo hayo yawe na matumizi mengine," alisema Ndaki.

Hata hivyo, aliwahimiza wawekezaji hao kuyatumia maeneo waliyowekeza kwa malengo yaliyokusudiwa na kwamba kuna baadhi ya wawekezaji hawayatumii vizuri maeneo hayo jambo linalosababisha kuvamiwa.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya NARCO, Paul Kimiti, alisema uvamizi unaoendelea unawaumiza wawekezaji na kuwakatisha tamaa huku akiiomba serikali kuchukua hatua kudhibiti vitendo hivyo.

Naiomba serikali kuangalia uwezekano wa NARCO kuwa na askari kama TANAPA, naamini watasaidia kudhibiti uvamizi huu kabla haujashamiri na vitendo hivyo vitakoma," alisema Kimiti.

Lengo la kikao hicho kilichoandaliwa na NARCO ni kuongea na wawekezaji hao kuhusu tozo mpya ya pango ya kitalu itakayoanza kutumika Julai 1, mwaka huu na kuwahimiza kuhuisha mikataba yao.




# Kunenge 'atwishwa' mzigo wa kero Chalinze

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

DIWANI wa Mbwewe, Omari Msonde, amemuomba mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, uandaliwe mkutano wa pamoja kati ya viongozi wa chama tawala, serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na Mahakama ili kutafuta suluhu kwa wakazi wa kata hiyo.

Msonde alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Madiwani na Mkuu huyo wa Mkoa, ambaye alikuwa akijitambulisha na kupokea kero ya kila kata ili zitafutiwe ufumbuzi

Alisema kuna malalamiko ya wafanyabiashara ya mkaa wakidai Wakala wa Misitu (TFS) kuwanyang'anya mizigo kwa madai ya kuvuna kinyume cha sheria na taratibu.

" Mkuu wa mkoa kwenye kata yangu hili la TFS imekuwa kero kubwa kwani ukifuatilia wapo wafanyabiashara ambao wana vibali vyote vinavyotakiwa, lakini bado wanakamatwa na mkaa wao kuchukuliwa na hao hao wanaowapa vibali, tusaidie kumaliza hili la kurudishwa amani," alisema Msonde.

Diwani huyo alielezea mgogoro mwingine ni isiyokwisha ya wakulima na wafugaji ambao umekuwa ukiibuka mara kwa mara wafugaji wanapolisha mifugo yao kwenye mashamba yenye mazao, na kwamba kesi ikifika mahakamani ndio wanashinda.

Naye Diwani wa Miono, Juma Mpwimbwi, alimuomba Mkuu huyo wa Mkoa kusaidia upatikanaji wa maji hususani maeneo ya vijijini ambapo kuna miradi haikamilika kwa wakati.

Kunenge alisema amepokea kero hizo, huku akiahidi kuzishughulikia kwa kushirikiana na viongozi wa mkoa, madiwani na watumishi wa halmashauri.

HABARI KITAIFA

# DUWASA yapata dawa ubambikizaji bili za maji

**NA Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), imekuja na mwarobaini wa ubambikizaji wa bili kwa kuanzisha mfumo shirikishi wa usomaji wa mita za maji.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa siku 100 za kujitathimini na uboreshaji wa huduma za upatikanaji wa maji na huduma kwa wateja.

Alisema DUWASA ni miongoni mwa mamlaka za maji zilizokuwa zikilalamikiwa kwa ubambikizaji wa ankara za maji na hivyo, waziri wa maji kuelekeza kutafuta mwarobaini wa kero hiyo.

Alisema walifanyia kazi maelekezo hayo kwa kuja na mfumo shirikishi wa usomaji wa dira za maji ambao mteja hupatiwa ankara ya maji ikiwa na namba zilizosomwa katika dira yake mwezi huo na zile za mwezi uliopita.

Alifafanua kuwa lengo ni kumpa mteja uwezo wa kuhakiki namba zilizopo kwenye dira yake kama zinaendana na zile alizotumiwa kwenye ankara ya maji na kujua ametumia maji kiasi gani akilinganisha na usomaji wa mwezi uliopita.

Alisema ankara hiyo pia huwekwa namba za mawasiliano ili kama mteja ataona tofauti aweze kuwasilina na mamlaka kwa ajili ya uhakiki zaidi.

Hata hivyo, alisema bado kuna mwitikio mdogo wa wateja kuhakiki dira zao kama zinaendana na ankara wanazotumiwa na kutoa wito kwa wateja wote kuhakiki dira zao kila wanatumiwa Ankara za maji ili kuondoa malalamiko ya kubambikizwa ankara kubwa.

"Tunaomba wateja wetu wote wawe wanahakiki dira zao wanapopata ankara za maji ambazo zinakuwa na namba zilizosomwa kwenye mita mwezi husika na mwezi uliopita zinazoonyesha kiasi cha maji aliyotumia," alisema Mhandisi Joseph.

# Mbuge aahidi kudhibiti magendo ya kahawa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, ameahidi kupambana na biashara haramu ya kutorosha kahawa kwenda nje ya nchi.

Alisema hayo wakati akizungumza na wadau wa zao la kahawa mkoani Kagera walioshiriki kikao cha uzinduzi wa mradi wa kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo kwa wakulima kilichoandaliwa na Cafeafrica nchini.

Mbuge alisema mkoa huo unategemea kahawa kama zao la biashara, na kwamba kuna jitihada za kuweka mikakati ya ulinzi ili kuzuia utoroshaji kwenda nchi jirani.

"Nitasimamia zao la kahawa kuvushwa kwenda nchi jirani ili iuzwe nchini na kuingiza kipato kwa manufaa ya kila mmoja na nchi kwa ujumla," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa kuna tija ndogo ya uzalishaji wa kahawa ya maganda shambani, na kwamba hekari moja inazalishwa kilo 1,200 hadi 1,600 badala ya 3,000 msimu huu.

Alisema ukusanyaji wa kahawa ya maganda kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulifika kilo 78,000 mwaka 2019/2020 uzalishaji wa zao hilo ulifikia kilo 92, 000.

Mkurungenzi Mtendaji wa Cafe Africa nchini, Dafroza Sanga, alisema mradi umelenga kunufaisha wakulima kwa miaka minne.

Alisema wilaya za Karagwe, Muleba na Kyerwa wakulima 6,881 walifikiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja ambao walipewa elimu ya jinsi ya kuanzisha mibuni inayozalisha kwa tija na uchipulishaji wa mibuni.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akiongea na Mbunge wa Monduli, Fredy Lowassa (kushoto), walipokutana katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kilichofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Mbunge huyo alikuwa ni miongoni mwa wawekezaji waliohudhuria kikao hicho. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Serikali yaunga mkono NMB mpango kuwezesha vijana kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amesema serikali inaunga mkono utaratibu wa kuwasaidia vijana kupitia jukwaa la huduma suluhishi za kibenki utakaowawezesha kifedha na kuwakwamua kiuchumi.

Utaratibu huo ulioanzishwa na Benki ya NMB unaojulikana kama "Go na NMB, alisema unaendana na sera za serikali za kuwashirikisha katika ujenzi na maendeleo ya taifa.

Katika hotuba yake ya kulizindua rasmi jukwaa hilo jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, Katambi alisema utaratibu huo umekuja wakati muafaka na ni uwekezaji stahiki.

"Hii ni kutokana na umuhimu na unyeti wa kada ya vijana kwenye shughuli za uzalishaji mali kwani wao ni raslimali watu ya msingi kiuchumi na katika maendeleo ya nchi kwa ujumla," alisema. Alisema lazima vijana wawe na ufahamu wa masuala ya pesa, wahusishwe kifedha, wasaidiwe kibiashara na kuwezeshwa kiuchumi.

"Jukwa la 'Go na NMB' ambalo ninalizindua rasmi leo linayazingatia hayo yote na ndiyo maana serikali inaliunga mkono kwani mikakati bunifu kama hii inatusaidia sana kuzikabili changamoto mbalimbali za vijana," alisisitiza.

Pia, alisema kuwa sifa kubwa ya jukwaa hilo ni kutobagua vijana watakaonufaika nalo kwa kuwa lipo kwa ajili ya vijana wote wa Kitanzania. Wawe ni wakulima, walioajiriwa ua kujiajiri na hata wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kawaida, wote watasaidiwa na kuhudumiwa, alisisitiza. Kwa upande wa NMB imesema jukwaa la "Go na NMB" ni maalumu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kibenki ya vijana lililoongezwa thamani kuwavutia ambalo litakuwa msingi wa kuwajenga na kuwapa uwezo wa kujitegemea kwa kuwapatia suluhishi za kifedha huku likitanguliza mbele maslahi yao pamoja na ndoto walizonazo.

"Moja ya malengo ya NMB katika hili ni kuwahudumia vijana kisasa zaidi na ni mpango mkakati wake kupanua wigo wa wateja kwa kujenga mazingira bora ya huduma za kibenki kwa vijana ili wao na benki hiyo waweze kuchangia kikamilifu ukuaji wa uchumi wa taifa."

Akizungumza kwenye tamasha la uzinduzi wa "Go na NMB" jijini Dar es Salaam, Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, alisema kila kijana ana haki ya kupata huduma salama inayofikika kwa urahisi na yenye tija.

"Dhamira yetu ni kutanua wigo wa huduma zetu ili tuwafikie vijana wote. Hii itawawezesha vijana wengi zaidi kufikiwa na huduma za kifedha huku ikiwasaidia kujenga utamaduni wa kuwa na nidhamu ya fedha wanapoandaa maisha yao ya baadaye hatua ambayo pia itakachangamsha uchumi wa nchi," alisema Mponzi.

Awali, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema faida na huduma wezeshi za kifedha za jukwaa la "Go na NMB" ni nyingi na zenye tija kimaendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Alisema huduma hizo ni pamoja na kujiunga kidijitali, kupata nafasi ya kushiriki promosheni na kujishindia zawadi zitakazokuwa zinatolewa kupitia vituo vya mauzo vya NMB pamoja na kupata mikopo nafuu ya bodaboda na pikipiki za miguu mitatu na bima.



Naibu waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara (kushoto), akimsikiliza Kaimu Meneja wa uwanja wa ndege wa Songwe, Wanje Juma, akieleza jinsi rada inavyofanya kazi wakati alipotembelea mtambo wa Rada wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania(TCAA), uliopo vilima ya Insuti wilaya ya Songwe. Naibu waziri Waitara amesisitiza kwamba kukamilika kwa mradi huo pamoja na miradi mingine miwili inayoendelea uwanjani hapo ya ukarabati wa eneo kurukia na uwekwaji wa taa ni sehemu ya maandalizi ya uwanja huo kuanza kufanya kazi masaa 24. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makala awapa makandarasi siri ya kupewa miradi

**Na Joseph Mwendapole**

MAKANDARASI wameshauriwa kuweka gharama za chini wanapoomba miradi ya ujenzi ili kuishawishi serikali kuachana na kutumia utaratibu wa force account na kuwatumia wao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, wakati akifunga mkutano wa mashauriano baina ya makandarasi na wadau wengine wa sekta ya ujenzi.

Mkutano huo wa siku mbili uliwakutanisha zaidi ya makandarasi 600 na wadau mbalimbali wa ujenzi ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Makala ambaye alimwakilisha Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, alisema iwapo makandarasi watabadilika basi kwenye mkoa wake atafanya nao kazi kwenye miradi mingi ya ujenzi wa miundombinu.

"Unakuta mradi ambao mkandarasi kaandika kwamba ataufanya kwa bilioni 2 mtu mwingine anakwambia anaufanya kwa Sh milioni 800... sasa hapo kama kiongozi unafanyaje, si inabidi uchukue wa milioni 800 kwa sababu serikali ina miradi mingi hivyo ingependa kuokoa fedha ili zifanye kazi zingine," alisema Makala

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa wakizembea wanapopewa miradi ya ujenzi, hali ambayo imeifanya serikali kuona umuhimu wa kufanya miradi hiyo kwa kutumia wataalamu wake na mafundi wa kawaida ili iishe kwa wakati.

Alisema wananchi wamekuwa wakikasirika sana wanapoona mkandarasi asiye na uwezo amepewa kazi na kujenga mradi kwa kiwango cha chini au kushindwa kuukamilisha kwa wakati.

Alisema hivi karibuni atazindua kampeni ya usafi hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kushirikisha makandarasi wazalendo, kwani taasisi kama Suma JKT haiwezi kufanya kazi za mkoa wote.

Alisema makandarasi watakaobahatika kupata kazi za serikali wazifanye kwa weledi na zikamilike kwa wakati ili waendelee kuaminika na kupewa kazi zingine za ujenzi serikalini.

Akisoma maazimio ya mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Mhandisi Consolata Ngimbwa, alisema makandarasi wameomba masharti ya mikopo yalegezwe na mikataba ya ujenzi itumike kama dhamana ya mikopo.

Alisema wameazimia kuwe na waranti pale malipo ya mkandarasi yanapocheleweshwa na serikali itenge miradi mbalimbali ya kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo ili wakuze mitaji yao wapate uwezo wa kujenga miradi mingi.

Ngimbwa alisema wameazimia kuwa uhaba wa kazi za ujenzi unatokana na kazi hizo kufanywa na taasisi za umma kama Suma JKT na TBA hivyo wameshauri serikali ijitoe na kuiachjia sekta binafsi kufanya kazi hizo.

# RC Mkirikiti: Kulipa Kodi si hiari, ni wajibu

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI mkoani Rukwa imewataka wananchi kupuuza uvumi ambao umeanzishwa na watu wachache wanaodai kuwa suala la kulipa Kodi ni mpaka mtu mwenyewe ajisikie, bali ni wajibu wa kila mwananchi na ni suala la kisheria.

Mkuu wa mkoa huo, Joseph Mkirikiti, ameyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na watendaji wa serikali.

Alisema kumekuwapo watu wachache ambao wanapotosha kwa kudai kuwa hivi sasa mwananchi kulipa Kodi ni mpaka ajisikie yeye mwenyewe, kitu ambacho alisema si kweli, kwani kulipa Kodi ni suala la kisheria.

Mkirikiti alisema hivi sasa serikali inatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na inahitaji fedha, hivyo ni lazima wananchi walipe kodi ili serikali ipate fedha za kutekeleza miradi hiyo.

"Nataka niwatahadharishe wanachi kuwa kulipa kodi ni wajibu na si suala la hiari, tulipe kodi ili serikali itekeleze miradi ya kimkakati pamoja na kujenga uwanja wa ndege wa hapa Sumbawanga, tusitegemee wafadhili tu, lazima na sisi tuchangie miradi hii," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Halfan Haule, alisema katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita, lazima kila mwananchi afanye kazi kwa bidii ili ajiletee maendeleo.

# 'Kodi taulo za kike imulikwe'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, ameitaka Mamlaka ya Mapato (TRA) kukaa na wafanyabiashara wa taulo za kike kuangalia upya namna ya kupunguza kodi zinazotozwa kwenye bidhaa hiyo, ili ipatikane kwa bei nafuu.

Alitoa agizo hilo juzi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani.

Alisema kwa sasa bidhaa hizo zinapatikana kwa gharama ambazo hazilingani na kipato cha wanawake wengi wa Kitanzania na wanashindwa kumudu kununua.

"Hali hii huwalazimu kutumia vifaa visivyo salama wakati wa hedhi na baadhi ya mabinti kutokwenda shuleni wakiwa kwenye hedhi," alisema.

Mwanaidi alisema bidhaa hizo zilizo nyingi zinazalishwa nje ya nchi na hivyo gharama za kuagiza zikiunganishwa na kodi hufanya bei iwe juu zaidi.

"Jambo hili ninaomba nishauri TRA kulitazama tena kwa mapana yake ili kupitia mamlaka zinazohusika kupendekeza namna ya kupunguza gharama za bidhaa za hedhi, zipatikane kwa bei nafuu," aliagiza.

Alisema TRA iendelee kuelimisha wafanyabishara ili kuzingatia bei elekezi kama ilivyo kwa bidhaa nyingine zinazopata bei elekezi serikalini.

Hata hivyo, alisema takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) juu ya masuala ya maji na usafi wa mazingira shuleni za mwaka 2018 zilizochapishwa Februari mwaka 2020, zinaonyesha hali duni ya huduma za hedhi.

Alisema asilimia 66.8 ya shule zote nchini ndiyo zina huduma ya hedhi salama na kati ya hizo zilizobainika na viteketezi ni asilimia 24 na zilizobaki ni asilimia 22.8 zinatupwa kwenye mashimo huku asilimia 19.5 zinachomwa kwenye vichomeo taka visivyokidhi viwango.

Aliwataka wasichana na wanawake kuzingatia hedhi salama ili kujiepusha na maambukizi ya magonjwa.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10 WALIONG'ARA ULAYA MSIMU WA 2020/21 UK. 12-13




FERNANDES

# WAPIGAJI PENALTI WATANO BORA EPL

## ISIKUPITE

MECHI tisa katika michezo 12, alizomaliza bila kuruhusu bao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, zinamfanya kipa wa Chelsea, Edouard Mendy, kufikia rekodi ya kucheza mechi nyingi kwenye michuano hiyo kwa msimu mmoja bila kuruhusu bao inayoshikiliwa na makipa (Santiago Canizares akiwa na Valencia msimu wa 2000-01 na Keylor Navas akiwa na Real Madrid msimu 2015-16).



**LONDON,** England

KUANZISHWA kwa teknolojia ya usaidizi wa marefarii kwa njia ya video (VAR) kwenye Ligi Kuu England, kumechangia kupatikana kwa penalti nyingi zaidi. Jumla ya penalti 118 zimetolewa kwa msimu huu 2020-21, zikiwa nyingi zaidi kuliko msimu wowote wa Ligi Kuu.

West Bromwich Albion ambayo imeshuka daraja, imetoa penalti nyingi zaidi msimu huu (10), ikifuatiwa na Manchester City (tisa). Shukrani kwa wapigaji wazuri wa penalti na imekuwa muhimu kwa timu nyingi.

Huku timu kama Brighton, zikijikuta kwenye wakati mgumu kutokana na kukosa penalti nyingi, timu kama Manchester United na Chelsea mabao yao mengi yametokana na penalti na kuwapa mafanikio.

Katika makala haya tunawaangalia wapiga penalti watano bora kwenye Ligi Kuu England (EPL), shuka nayo sasa...

### #5. HARRY KANE

Ametwaa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora katika Ligi Kuu England msimu huu na amefunga penalti saba katika mashindano yote kwa klabu na nchini msimu huu wa 2020-21.

Kane ni mmoja wa mastraika bora wa Tottenham Hotspur na England ambaye ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu. Katika mechi 48 alizocheza kwenye mashindano yote, nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, amehusika katika mabao 48 (akifunga 32, na kutoa pasi za mwisho 16).

Spurs imekuwa na msimu mbaya zaidi katika siku za hivi karibuni, lakini Kane na Son-Heung Min wameipa mafanikio makubwa timu hiyo kwa kuiwezesha kufuzu mashindano ya Ulaya msimu ujao.

Kane amefunga penalti 44 katika maisha yake ya soka la kulipwa na amekosa saba tu. Amekuwa na asilimia 100% katika uwiano wa kufunga penalti kwa msimu wa Ligi Kuu England 2020-21.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, msimu huu amefunga mabao 22 ya ligi katika mechi 34, yakiwamo manne ya penalti.

### #4. JORGINHO

Mzaliwa wa Brazil raia wa Italia, Jorginho na ndiye mfungaji bora wa Chelsea kwenye ligi msimu huu wa 2020-21, akifunga mabao saba yote kwa penalti. Jorginho alifunga penalti mbili dhidi ya Crystal Palace mapema msimu huu.

Katika mechi 41 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu, Jorginho amehusika katika mabao kumi.

Wakati nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, anaweza kufurahia kuwa na kiwango kizuri cha kufunga msimu huu, lakini Jorginho amekosa penalti tatu, mara mbili kwenye Ligi Kuu na moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi. Kiungo huyo alikosa penalti dhidi ya kipa Alisson na Bernd Leno, ambapo matokeo yalikuwa ni ya kipigo cha 2-0 na 3-1.

### #3. JAMIE VARDY

Ni straika wa Leicester City, Jamie Vardy ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka kadhaa iliyopita.

Vardy amefunga mabao saba (sita kwenye Ligi Kuu) kwa penalti msimu huu. Leicester City imekuwa ikiondoka na ushindi kila Vardy anapofunga kwa penalti na amekosa moja tu kwenye ligi msimu huu dhidi ya kipa wa Wolves, Rui Patricio.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao 26 kwa penalti katika kipindi chake cha uchezaji. Amekosa penalti tano tu tangu alipopewa jukumu la kuwapigia penalti 'Mbweha' hao msimu wa 2015-16.

Katika mechi 41 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu, Vardy amefunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho tisa.

### #2. MOHAMED SALAH

Mohamed Salah amekuwa na msimu mwingine wa kuvutia akifunga mabao 22 msimu huu kwenye Ligi Kuu England 2020-21. Nyota huyo wa kimataifa wa Misri amefunga jumla ya mabao 31 na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 50 alizocheza kwenye mashindano yote kwa Liverpool msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amefunga mabao saba kwa penalti msimu huu wa 2020-21, yakiwamo saba ya Ligi Kuu. Salah alifunga 'hat-trick' ya kukumbukwa dhidi ya Leeds United mapema msimu huu na kuisaidia Liverpool kupata ushindi wa mabao 4-3, akifunga penalti mbili. Ni mshindi mara mbili wa Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu England.

### #1. BRUNO FERNANDES

Bruno Fernandes amekuwa mpigaji bora wa penalti kwa Manchester United, akifunga 13 kati ya 14 alizopiga.

Manchester United imepoteza mara mbili tu wakati Fernandes alipofunga penalti. Raia huyo wa Ureno, amewafunga magolikipa 12 tofauti msimu huu akiwamo Keylor Navas, Ederson, Emiliano Martinez na Illan Meslier.

Golikipa wa Newcastle United, Karl Darlow, ndiye kipa pekee aliyeokoa penalti ya Fernandes msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amefunga penalti tisa kwenye Ligi Kuu England msimu huu. Fernandes amefunga penalti 21 kwa United katika mashindano yote.

## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIONG'ARA ULAYA MSIMU WA 2020/21


HAALAND

**LONDON,** Egland

LIGI Kuu barani Ulaya zimefikia mwisho na sasa nguvu inaelekezwa kwenye michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020. Kumekuwa na kiwango cha kuvutia kwa wachezaji kwa msimu huu 2020/21.

Wakati wachezaji nyota wameendelea kuimarisha viwango vyao, wachezaji wengine vijana wameendelea kuwa na wakati mzuri wa kuelekea kuwa magwiji wa baadaye.

Katika makala haya, tunawaangalia wachezaji 10 barani Ulaya ambao walikuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu kwa mujibu wa takwimu(2020/21), twende sasa...

**#10. ERLING BRAUT HAALAND (BORUSSIA DORTMUND) | 7.58**

Mmoja wa mastraika bora duniani, Erling Braut Haaland tayari ni nyota akiwa na umri wa miaka 20. Akiwa amejenga jina lake kule Red Bull Salzburg, Haaland alijiunga na Borussia Dortmund Januari 2020 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 18.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amecheza mechi 27 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu, akifunga mabao 25 na kutoa pasi za mwisho sita. Manchester United, Manchester City, Real Madrid, Chelsea na Barcelona zote zinahusishwa na kuhitaji huduma ya straika huyo.

**#9. JACK GREALISH (ASTON VILLA) | 7.59**

Jack Grealish ni mchezaji wa aina yake, ni ngumu kwa Aston Villa kubaki naye kwa msimu ujao. Zao la akademi ya Aston Villa, Grealish ni nahodha wa klabu hiyo na mchezaji huyo wa kimataifa wa England uwezo wake dimbani ni wa kiwango cha juu na msimu huu umekuwa bora zaidi kwake chini ya kocha, Dean Smith.

Grealish alisaini mkataba wa muda mrefu kubakia hapo Aston Villa mwaka jana na kwa vyovyote atagharimu fedha nyingi kwa klabu yoyote itakayomtaka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye amecheza mechi 25 za Ligi Kuu England msimu huu na kufunga mabao sita, ametoa pasi za mwisho 10 na amekuwa akihusishwa sana na Manchester United, Manchester City na Arsenal.

**#8. LORENZO INSIGNE (NAPOLI) | 7.59**

Ni mchezaji ambaye hasemwi sana, Lorenzo Insigne amekuwa na kiwango kisichoshuka pale Napoli na yupo kwenye kikosi cha kwanza.

Insigne ametumia muda wake mwingi zaidi kucheza hapo Napoli, baada ya kucheza kwa mkopo Cavese, Foggia na Pescara. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaweza kucheza winga ya kushoto au straika, amekuwa na msimu wa kuvutia na ndiye mchezaji bora wa Napoli kwa sasa.

Mkataba wa sasa wa Insigne na Napoli unamalizika mwaka 2022, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia, amecheza mechi 34 za Serie A msimu huu, akifunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho saba.

**#7. ANDY DELORT (MONTPELLIER) | 7.60**

Andy Delort amekuwa na wakati mzuri zaidi pale Montpellier na msimu huu bila shaka yoyote umekuwa bora zaidi kwake.

Delort alijiunga na Montpellier kutoka Toulouse mwaka 2018 kwa mkopo, kabla ya kusaini mkataba wa kudumu mwaka 2019 kwa ada ya pauni milioni milioni. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria ameonyesha ubora wake hapo Montpellier.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye awali alitumia muda wake kucheza na Wigan Athletic, amecheza mechi 29 za Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, akifunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho tisa. Delort ni mmoja wa wachezaji wawili wanaotoka Ligue 1 katika orodha hii.

**#6. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS) | 7.61**

Juventus imemaliza msimu vibaya ikiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa Serie A.

'Kibibi Kizee' hicho cha Turin mchezaji wake nyota ni Cristiano Ronaldo, ambaye ameonyesha kiwango cha kuvutia. Ndiye mfungaji bora wa ligi hiyo msimu huu. Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, anatajwa kwamba anataka kuondoka nchini Italia.

Uvumi umekuwa ukisambaa kwamba anaweza kurudi Manchester United, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu Marekani (MLS), zikimkodolea macho.

**#5. GERARD MORENO (VILLARREAL) | 7.64**

Kama Andy Delort, Gerard Moreno amefurahia msimu wa kuvutia akiwa na Villarreal, amebeba Kombe la Ligi ya Europa.

Akiwa ameaanza kucheza soka la kulipwa hapo Villarreal, Moreno alitengeneza jina lake kule Espanyol kabla ya kurudi Villarreal mwaka 2018 kwa ada ya pauni milioni 18. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na msimu wa kuvutia. Straika huyo ana uwezo wa kucheza winga ya kushoto na amekuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha Unai Emery.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, amecheza mechi 32 za Ligi Kuu akifunga mabao 23 na kutoa pasi za mwisho sita. Barcelona inatajwa kumuwania Moreno.

**#4. KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN) | 7.68**

Ni mchezaji wa pili kutoka Ligue 1 katika orodha hii, ambaye anatamba pale, Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora duniani kwa sasa ameshapata mafanikio makubwa katika umri wake huo mdogo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia na miamba wa Paris, huku Real Madrid na Liverpool zikionekana kumtolea macho. Paris Saint-Germain ilimsajili kwa pauni milioni 130.5 kutoka AS Monaco.

**#3. HARRY KANE (TOTTENHAM HOTSPUR) | 7.76**

Ni mchezaji bora wa Ligi Kuu England, Harry Kane akitamba pale Tottenham.

Majaliwa ya Kane kuendelea kuwapo hapo Tottenham Hotspur ni madogo hasa baada ya timu hiyo kuwa na msimu mbaya. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amebainsisha wazi kwamba baada ya msimu huu wa 2020/21 anataka kwenda kutafuta changamoto nyingine kwingineko.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amecheza mechi 34 za Ligi Kuu England akifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 13.

**#2. ROBERT LEWANDOWSKI (BAYERN MUNICH) | 8.03**

Mmoja wa wachezaji bora duniani na pia straika bora kabisa katika kizazi cha sasa, Robert Lewandowski.

Bayern Munich walimsajili Lewandowski akiwa huru mwaka 2014 na amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amecheza mechi 328 katika mashindano yote kwa 'Bavaria' hao, akifunga mabao 293. Ameshinda mataji saba ya Bundesliga akiwa Bayern Munich na alikuwa mchezaji muhimu sana msimu uliopita walipobeba Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu huu Lewandowski amecheza mechi 29 za Ligi Kuu Bundesliga, akifunga mabao 41 na kutoa pasi za mwisho saba.

**#1. LIONEL MESSI (BARCELONA) | 8.52**


Mchezaji bora zaidi kuwahi kushuhudiwa kwenye ulimwengu wa soka, Lionel Messi na ndiye mchezaji bora zaidi Ulaya kwa mujibu wa takwimu kwa msimu huu.

Mfungaji, mtoa pasi na katika umri wake wa miaka 33, ameendelea kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Barcelona.

Mkataba wa Messi na Barcelona unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto na kwa sasa Rais, Joan Laporta anapambana kuhakikisha anambakiza. Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amecheza mechi 35 za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu akifunga mabao 30 na kutoa pasi za mwisho tisa. Messi amekuwa akihusishwa sana na Manchester City na Paris Saint-Germain tangu msimu uliopita.

## Nukuu

"Nilianza kupenda kubadilishana jezi au zawadi wakati umri umenitupa mkono, sikuzingatia hilo hapo awali. Ninajuta kwa kutokuomba jezi kutoka kwa wachezaji ambao nimekutana nao nilipokuwa kinda na kuanza - kama vile Ronaldo [R9] de Lima au Roberto Carlos. Ningependa kuwa na jezi zao, " **Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi**



"Nilifanya uchaguzi sahihi wa kikosi cha ushindi. Kama msimu uliopita dhidi ya Olympique Lyon, kama ilivyokuwa dhidi ya PSG na Dortmund, wachezaji wanalijua hilo," **Kocha wa Machester City, Pep Guardiola, akijitetea baada ya kuulizwa swali na waandishi wa habari kuhusu uteuzi wake wa kikosi kilichopigwa bao 1-0 na Chelsea kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi.**



"Ahsante Maestro [Andrea Pirlo], ni heshima kunolewa na wewe," **Cristiano Ronaldo alitupia ujumbe huo Ijumaa katika mtandao wake wa Instagram ukiambatana na picha ya pamoja ikiwa ni baada ya saa moja Juventus kumtimua kocha huyo na kutangaza kurejea kwa Massimiliano Allegri.**






# BOCCO NA UTAMU WAKE MABAO 132 LIGI KUU

Nahodha wa Simba, John Bocco, akishangilia bao la pili alilofunga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC katika Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, timu yake ikishinda 3-1 juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwangwo**

NI bao lililokuwa likisubiriwa na mashabiki wengi wa Simba kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi juzi. Baada ya kuwa nyuma kwa bao moja kwa kipindi kirefu, Simba ilisawazisha kupitia kwa Chris Mugalu dakika ya 78.

**Hata hivyo, kiu ya wanachana na mashabiki wengi wa Simba ilikuwa ni kushinda mechi hiyo ili kuwa mbali kwa pointi na mahasimu wao wa jadi, Yanga.**

Ndipo nahodha John Bocco alipoliongoza vema jahazi lake kwa kupachika bao la pili dakika ya 83, ambalo si tu lilishangiliwa kwa nguvu na wanachama na mashabiki wa Simba nchi nzima, lakini hata yeye mwenyewe alilishangilia kana kwamba lilikuwa ni bao lake la kwanza tangu aanze kucheza Ligi Kuu.

Ukweli ni kwamba Bocco alikuwa anafunga bao la 132 yakiwa ni ya Ligi Kuu tu kwa misimu 13, tangu aanze kucheza msimu wa 2008/09. Hayo ni ya kwenye Ligi Kuu, achilia mbali Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la FA, michuano mingine mbalimbali na mechi za kirafiki.

"Nawapongeza wachezaji wenzangu kwa kupambana hadi tumepata ushindi. Haikuwa rahisi kwa sababu wenzetu walitutangulia. Niwapongeze nao kwa sababu wamecheza vizuri ndiyo maana mechi ilikuwa ngumu sana. Nawapongeza pia mashabiki wetu wa hapa na waliosafiri kuja kutuunga mkono," alisema nahodha huyo na kuongeza.

"Ndiyo wanasema thamani yangu inaongezeka, lakini mimi najituma zaidi kwa ajili ya kuisaidia timu yangu," alisema.

Bocco ndiye straika pekee aliyebaki kwenye kiwango kile kile au kuzidi kuliko wote alioanza nao msimu huo na hata wengine baada ya hapo.

Ndiye straika pekee Mtanzania ambaye kocha yeyote anaweza kuwa na mategemeo ya kupata mabao 10 kwake kwa msimu mmoja.

Kwa sasa Bocco ndiye straika aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu kati ya mastraika wote wanaoendelea kucheza naye. Na kwa jinsi anavyocheza na kiwango chake, anaonekana ataendelea kuzifumania nyavu tena na tena.

Ni mchezaji ambaye kila miaka inavyozidi kusonga mbele, thamani yake inaongezeka na kuzidi kuwaacha mbali mastraika vijana ambao kasi yao inakuwa kama maji ya bahari, kupwa na kujaa.


Bao alilofunga juzi lilikuwa ni la 11 msimu huu, akiwa sawa na straika mwenzake wa Simba, Meddie Kagere. Ni pungufu ya mabao matatu juu ya kinara wa ufungaji wa Ligi Kuu kwa sasa, Prince Dube wa Azam ambaye ana mabao 14.

Mara nyingi nahodha huyo amekuwa akisumbuliwa na majeraha na ameanza kurejea dimbani hivi karibuni baada ya kuwa nje kutokana na kuwa majeruhi. Wengi wanasema kama si majeraha angeweza kuwa na mabao mengi zaidi.

Muda mfupi tu baada ya kurejea, ameifungia Simba mabao matano kwenye mechi tatu tu alizocheza. Mawili ni dhidi ya Kaizer Chiefs, Simba ikishinda 3-0 Ligi ya Mabingwa Afrika, mawili ni kwenye Kombe la FA dhidi ya Dodoma Jiji, timu yake ikishinda 3-0, kabla ya bao hilo kwenye mechi ya Ligi Kuu.

Kati ya mabao hayo 132 ya Ligi Kuu, 82 ameifungia Azam FC, huku Simba akifunga mabao 50, tangu ajiunge nayo msimu wa 2017/18.

## JE, WAJUA?



KOCHA Pep Guardiola amepoteza mechi nyingi (nane) dhidi ya Chelsea katika mashindano yote kuliko dhidi ya klabu yoyote ile, kati ya hizo amepoteza mara tatu mfululizo dhidi ya 'Blues' hao. Aidha, timu nyingine ambayo amepoteza michezo mitatu mfululizo dhidi yake katika kazi yake ya ukocha ni Real Madrid (msimu wa 2012-14) na Liverpool (2018).



# Mulamula afunguka uhusiano Tanzania na jumuiya ya kimataifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema kuwa uhusiano wa Tanzania kikanda na kimataifa yanaendelea kuimarishwa katika maeneo mbalimbali.

Balozi Mulamula, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na watumishi wa Wizara yake kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.

Alisema kuwa lengo kuu ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa mstari wa mbele katika masuala ya kuimarisha amani, uhuru, na maslahi ya Taifa katika nyanja za kimataifa ikiwa ni pamoja na kutumia fursa za kiuchumi zitokanazo na uhusiano huo.

Aidha, alisema katika diplomasia ya siasa, Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaelekeza kuboresha utekelezaji wa mipango ya kuimarisha diplomasia ya siasa ya kimkakati kwa ajili ya kulinda amani, uhuru, maslahi ya taifa na kuimarisha ujirani mwema.

Pia, alisema kuboresha na kuimarisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine na taasisi za kimataifa ikiwa ni pamoja na sauti ya Tanzania na taswira yake katika medani ya uhusiano wa kikanda na kimataifa.

"Katika diplomasia ya kiuchumi pamoja na mambo mengine, kazi yetu ni kukuza mahusiano ya kiuchumi na mataifa, jumuiya za kikanda na taasisi nyingine za kimataifa, kulinda uchumi na masilahi mapana ya Taifa kwa kutumia jiografia ya nchi kimkakati na ushawishi wa kihistoria, hususan kwenye ukanda wa Kusini."

"Kuhakikisha kuwa balozi zetu zinakuwa kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zetu," alisema Balozi Mulamula.

Alisema kuwa ilani haikuacha kuipa Wizara majukumu ya kimtambuka, hivyo imeorodhesha masuala mtambuka ambayo yanatakiwa kuyafanywa ikiwa ni pamoja na ushiriki kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, (SADC), Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, umoja wa nchi zisizofungamana na upande wowote na Jumuiya nyingine za kimataifa.

"Ndugu watumishi ili haya yote yatekelezwe, uongozi wa wizara, watumishi na balozi zetu lazima zijipange kimkakati kutekeleza majukumu yote tuliyopewa,"alisema.

Vilevile, alisema katika kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa ufanisi, chini ya uongozi wao wana dhamira ya dhati ya kujenga nguvu ya pamoja na kuhakikisha kuwa wizara, balozi na taasisi za wizara zinafanya kazi kwa ukaribu na ushirikiano wa hali ya juu.

Hata hivyo, alisema utendaji wa wizara hiyo katika miaka michache iliyopita haukuwa wa kuridhisha.

Alisema hali hiyo ilitokana na ukweli kuwa Ikama ya wizara haijafikiwa kama inavyotakiwa, balozi zimekuwa zikihangaika kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya kutokuwa na watumishi wa kutosha na vitendea kazi.

Alisema kutokana na maelekezo ya Rais, wanakamilisha kupeleka watumishi kwenye balozi kulingana na uwezo wa kifedha wa serikali.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza na wabunifu wa Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, alipotembelea Banda la Chuo hicho kwenye Maonyesho ya Pili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yanayoendelea katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **PICHA: ANTHONY SIAME**

## Wanafunzi elimu ya juu wamuahidi Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMUIYA ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (TAHLISO), imemuahidi Rais Samia Suluhu Hassan kuwa vyuo vitaendelea kuwa salama kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali.

TAHLISO imesema miongoni mwa jitihada hizo ni kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi.

Mwenyekiti Mstaafu wa Jumuiya hiyo, Peter Niboye, aliyasema hayo jijini hapa katika hafla ya kuapishwa viongozi wapya wa TAHLISO waliochaguliwa Mei 23, mwaka huu.

Alisema kuna jitihada mbalimbali zimefanywa na serikali za kuhakikisha Watanzania wa hali ya chini wanapata elimu ya juu, ikiwamo kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu hadi kufikia Sh. bilioni 500 kwa wanafunzi wa 2021/2022.

"Tunamshukuru Rais Samia na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa kutulea sisi vijana na kuonyesha weledi mkubwa katika kusimamia misingi ya nchi, kukuza uchumi na kuendelea na ujenzi wa miradi mingi ya kimkakati...sisi wanafunzi wa elimu ya juu na kati tunasema ahsanteni sana, na tunaimani kubwa sana nao," alisema.

Akielezea mafanikio ya TAHLISO, alisema imekuwa kiunganishi kikubwa kati ya wanafunzi na serikali, imedumisha hali ya amani vyuoni na kuwasilisha changamoto na kutatuliwa kwa wakati, na kwamba imekuwa daraja kubwa la kulinganisha kati ya serikali na wanafunzi.

"Suala la migomo limeondoka kabisa, kwa muda wote tumehubiri amani, uzalendo na vijana kuisemea mazuri ya serikali. Ni Imani yetu kuwa jukumu hili litaendelea na niwaombe wenzetu waendelee kuwa mabalozi wema ndani na nje ya nchi," alisema.

Naye, Mwenyekiti mpya wa jumuiya hiyo, Frank Nkinda, aliziomba menejimenti za vyuo vikuu kuondoa kero ambazo zimekuwa mwiba kwa wanafunzi na kusababisha viongozi wa serikali za wanafunzi kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Aidha, alisema katika uongozi wake atahakikisha suala la kurudia mitihani sio sehemu ya maisha ya wanafunzi wa vyuo.

Aliwashukuru viongozi waliomaliza muda wao kwa kutatua kero zilizokuwapo kwenye baadhi ya vyuo na kusimamia maslahi ya wanafunzi.

Naye, Makamu Mkuu wa Chuo cha Mipango (Taaluma ya Utafiti), Dk. Provident Dimoso, aliipongeza uongozi uliopita kwa kutatua kero ya bima za afya kwa wanafunzi.

## Madiwani wataka kusambazwa kwa kondomu za kike

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

KATIKA kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU), Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, imeombwa kusambaza kondomu za kike ili kuwalinda wanawake na maambukizi.

Rai hiyo ilitolewa na madiwani wa viti maalum wa halmashauri ya wilaya hiyo wakati wakijadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na kamati ya kudhibiti UKIMWI kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika Chamwino.

Diwani wa Viti Vaalum, Edina Mwachitu, alisema pamoja na jitihada zilizofanywa na halmashauri hiyo kusamba kondomu za kiume kwenye kata zote, ni vyema zikafanywa na kwa wanawake ili kuwakinga na maambukizi hayo.

"Hii huduma itolewe kwa jinsia zote ili tutokomeze maambukizi ya VVU kwenye maeneo yetu, kwa kuwa wanawake walio wengi wanaweza kukaa majumbani kuliko kinababa, ambao baadhi yao ni wanywaji wa pombe na wanaporudi majumbani wanakuwa wamelewa na hawataki kutumia hizo kondom kwa madai ya wao wanataka waaminiwe tu," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Kenneth Yindi, alisema kondomu zinazosambazwa ni za kiume peke yake.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kamati hiyo kwa miezi mitatu, Yindi alisema kuna kila sababu kwa Halmashauri hiyo kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali kupambana na maambukizi hayo kwa kusambaza kondomu hizo.

"Tumesikia kilio chenu na halmashauri na taasisi zinginezo zinazojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI, itahakikisha kondomu hizo kwa ajili ya wanawake pia zinasambazwa kwa ajili ya kujilinda maambukizi ya virusi hivyo," alisema.

Alisema hadi sasa maboksi ya kondomu 10,200 yamesambazwa kwenye kata 25 za wilaya hiyo.

"Hii imeenda sambamba na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi katika maeneo mbalimbali ikiwamo miradi ya ujenzi wa barabara kuanzia vitongoji,vijiji,kata hadi wilaya.



# Uchaguzi Zambia wasitisha majadiliano ya reli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAZUNGUMZO ya kuboresha reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) yamekwama kuendelea kutokana na mchakato wa Uchaguzi Mkuu unaoendelea nchini Zambia.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea karakana ya kukarabati vichwa vya treni iliyopo eneo la Iyunga jijini Mbeya.

Alisema kuwa kwa sasa reli hiyo inahitaji kufanyiwa maboresho makubwa, lakini kutokana na sheria inayounda Shirika hilo, Serikali ya Tanzania haiwezi kutekeleza maboresho hayo mpaka ifikie makubaliano na Serikali ya Zambia.

"Reli hii inahitaji kufanyiwa maboresho makuwa, lakini kama mjuavyo reli hii inamilikiwa na Shirika letu TAZARA ambalo kisheria linamilikiwa na nchi mbili za Tanzania na Zambia, kutokana na sheria hiyo sisi Watanzania hatuwezi kufanya maboresho hayo mpaka tukubaliane na wenzetu wa Zambia," alisema Waitara na kuongoza

"Tulishaanza mazungumzo ya kulifanyia shirika hili maboresho yanayohitajika, lakini kabla hatufikia makubaliano, wenzetu wa Zambia wakaingia kwenye mchakato wa uchaguzi na hivyo mazungumzo yetu yakasimama, hivi sasa tunawasubiri wamalize uchaguzi ili apatikane waziri wa Uchukuzi kwa upande wao ndipo tukamilishe mazungumzo yetu," alisema Waitara.

Aliyataja baadhi ya mambo yanayohitaji maboresho kwenye reli hiyo ni kuongeza idadi ya vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na abiria pamoja na uwezo wa reli hiyo kusafirisha mizigo mingi zaidi.

Meneja wa Tazara Mkoa wa Tanzania, Mhandisi Fuad Abdallah, alisema kuwa zamani shirika hilo lilikuwa likimiliki vichwa vya treni zaidi 102, lakini kwa sasa idadi hiyo imeporomoka na kusalia vichwa 14 tu vinavyofanya kazi.

Alisema ili reli hiyo iongeze uwezo wake wa kusafirisha mizigo, inatakiwa vichwa vya treni viongezeke sambamba na mabehewa ya mizigo.

"Tunahitaji kuongeza uwezo wa reli yetu wa kusafirisha mizigo na hata abiria, lakini ili suala hili lifanikiwe inatubidi tuongeze vichwa vya treni na mabehewa, jukumu hili ni la serikali za Tanzania na Zambia kwa pamoja maana wao ndio wamiliki wa shirika hili," alisema Abdallah.

Alisema shirika mwaka 2014 lilikuwa na uwezo wa kusafirisha mizigo tani 85,000 lakini kwa sasa uwezo huo umeongezeka na kufukia tani 400,000 kwa mwaka.

Alisema hali hiyo imesababishwa na ufufuaji wa vichwa vya treni vilivyokuwa vimekufa na kwamba wanaendelea na jitihada za kuongeza uwezo wa kusafirisha mizigo hadi kufikia tani 800,000 kwa mwaka katika kipindi kifupi kijacho.

Alisema kuwa asilimia 80 ya shaba yote inayozalishwa katika nchi za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa sasa zinasafirishwa kupitia reli ya TAZARA.

Kwa upande wake Meneja wa Karakana ya TAZARA, Mhandisi Ezekiel Mong'ateku, alisema matengenezo ya Reli hiyo awali yalikuwa yanafanywa na raia wa China ambao ndio waanzilishi wa Reli hiyo lakini kwa sasa kazi hizo zinafanywa na wazawa.

Alisema kwa sasa Karakana hiyo ina wafanyakazi 69 ambao 55 kati yao ni Watanzania ambao wamechukuliwa kutoka katika vyuo mbalimbali vya Ufundi Stadi (VETA) na 14 ni raia wa Zambia.

Reli ya Tazara ni miongoni mwa mashirika ambayo yalikuwa na hali mbaya kabla ya mwaka 2015 kutokana na usimamizi wake kuwa mbovu lakini kwa sasa Shirika hilo limeanza kuimarika.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akiangalia baadhi ya Nyaraka zinazohusu Mkataba kati ya mmoja wa wamiliki wa Leseni za uchimbaji wa madini ya dhahabu kwenye Kijiji cha Mlima Njiwa na mwekezaji wa eneo hilo, wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipotembelea kijiji hicho kwa ajili ya kutatua mgogoro uliopo kati ya pande hizo mbili. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Homera aanza na huduma za afya kwa wazee

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewapa siku 14 wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo kuandaa madirisha maalumu kwa ajili ya kuhudumia wazee kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao na wawakilishi wa wazee kutoka wilaya zote za mkoa huo, ambapo alisema baada ya siku hizo kumalizika atafanya ziara ya kukagua madirisha hayo kwenye vituo hivyo.

Alisema baada ya siku hizo kuisha hatataka kuona wazee wanapanga foleni kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, kutamkiwa lugha mbaya wala kutakiwa kwenda kununua dawa kwenye maduka ya watu binafsi, kwa maelezo kuwa Serikali inapeleka dawa kwa ajili ya kundi hilo kwenye vituo hivyo.

"Haiwezekani wazee wetu wamelitumikia taifa letu kwa uzalendo halafu wawe wanapata shida, sio mzee ana kitambulisho kinachomtaka atibiwe bure halafu anasimama kwenye foleni, kila muda anaambiwa subiri inaweza ikafika muda mzee akaanguka, sasa sihitaji mambo hayo," alisema Homera.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo mbalimbali na kuwachukulia hatua kali vijana wote ambao hawafanyi kazi, badala yake wanacheza michezo isiyoruhusiwa kuchezwa mchana.

Alisema baadhi ya vijana hao ndio wanaofanya matukio ya unyanyasaji dhidi ya wazee ikiwamo kuwaibia, kuwapiga na hata kuwatamkia maneno machafu.

Alisema baadhi ya vijana hao huwa wanavuta bangi na kutumia dawa zingine za kulevya, hali ambayo inachochea vitendo vya uharifu kwenye jamii.

Katika hatua nyingine, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya kushirikiana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuboresha barabara, huku akilitaka Jiji la Mbeya kutenga Sh. bilioni moja kila mwaka.

Awali baadhi ya wazee wa Mkoa huo, waliiomba Serikali iwasaidie kuwadhibiti vijana wao kwa maelezo kuwa baadhi wamekuwa wavivu kufanya kazi na badala yake wanashinda wakicheza kamari.

Mmoja wa wazee hao, Halima Mwakitalima kutoka katika Kata ya Ilemi, alisema baadhi ya vijana wao wanavuta bangi na kunywa pombe kali za moshi (gongo) na wakirejea nyumbani wanaanza kuwapiga wazazi wao bila sababu.

"Tunaomba mtusaidie maana hatuna amani kabisa, watoto wetu wanakunywa sana pombe na kuvuta mibangi na wakifika nyumbani wanaanza kutupiga na kutudhalilisha wazazi wao," alisema Halima.

Kwa upande wake mzee Hosea Osasine kutoka katika Wilaya ya Mbarali, alimuomba Mkuu wa Mkoa kuwasaidia kutatua migogoro ya ardhi katika kwa maelezo kuwa wazee ndio wanaoathirika zaidi.

Alisema baadhi ya migogoro inayowatesa wananchi wa Mbarali ni ya wakulima na wafugaji, wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na migogoro ya wakulima wadogo na wawekezaji wa mashamba makubwa.

## Wazazi waonywa kusambaza picha za watoto mitandaoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi mkoani Mbeya wameonywa kuacha kusambaza mitandaoni picha za watoto wao, kwa madai kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria na ni ukatili wa kimtandao ambao huathiri kundi hilo.

Vilevile wametakiwa kuepuka kuwaacha watoto wenye umri mdogo watumie vifaa kama simu na kompyuta, na kwamba hata wakitumia vifaa hivyo wanatakiwa wavitumie chini ya usimamizi wa wazazi na walezi.

Mwakilishi wa Dawati la Jinsia kutoka Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Emmakulata Mwalanda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha jijini Mbeya, ambapo alisema ukatili wa kimtandao umekuwa tishio kipindi hiki cha maendeleo ya Teknolojia.

"Ukatili wa kimtandao ni aina ya tano ya ukatili wa kijinsia, ukiacha ule ambao tumeuzoea ambao ni ukatili wa kingono, kimwili, kisaikolojia na kiuchumi, aina hii mpya ya ukatili imezidi kukua kwenye jamii zetu huku wazazi na walezi wakichukulia jambo hilo kuwa la kawaida," alisema Emmakulata

Aliwatadaharisha wazazi kuweka mbali vifaa vya mawasiliano au kuviwekea nywila ili kuwaepusha watoto wao wasivichezee na kuangalia vitu vilivyomo humo akionya kuwa baadhi havina maadili.

Akizungumza wakati wa mahafali hayo mkuu wa chuo, Mhandisi Hassan Kalima alisema zaidi ya vijana 8900 walijitokeza kuomba nafasi ya mafunzo ya ufundi wa fani mbalimbali katika chuo hicho ambayo yanafadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema maombi ya mafunzo hayo ambayo yalihitimishwa Aprili 30, mwaka huu yalionyesha namna vijana walivyokuwa na ari pamoja na mwamko wa kupata mafunzo stadi kwenye vyuo ambavyo vilianishwa na serikali.

"VETA Mbeya tulipokea maombi 8995 kwa ajili ya mafunzo yaliyofadhiliwa na serikali, lakini waliorejesha fomu walikuwa ni 6,900, na sasa bado tunaendelea na mchakato, lakini kwa taarifa nilizopata ni kwamba vijana wote walioomba watafikiwa na wataendelea kupata mafunzo stadi ya ufundi" alisema



# ‘Uhuru wa habari unajenga demokrasia’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema kuwapo kwa uhuru wa habari kunasaidia kujenga demokrasia ya kweli ambayo husaidia kuimarisha utawala bora, uwazi na uwajibikaji.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari ulioambatana na tunzo za umahiri wa waandishi wa habari Zanzibar, uliofanyika mjini hapa.

Alisema kutokuwapo kwa uhuru wa habari kuna maana moja tu, nayo ni kukandamizwa kwa demokrasia ambayo ni kichocheo cha maendeleo, haki na uwajibikaji.

“Nchi nyingi ikiwamo Tanzania zinafahamu umuhimu wa uhuru wa habari na ndio maana Katiba ya Tanzania pamoja na Katiba ya Zanzibar kifungu cha 18, zimeelezea kwak ina dhana na umuhimu wa uhuru wa habari.

Alikiri kuwapo vifungu vya Katiba vinavyotoa uhuru wa habari katika katiba za nchi nyingi, haina maana kuwa uhuru huo wa habari haupo.

Aidha, alisema kuwa baadhi ya waandishi wa habari katika nchi nyingi wamechochea balaa na kusababisha maafa yasiyosahaulika na kuwasisitiza kufanya utafiti na kuhakikisha wanatoa habari sahihi.

Alisema bado kuna upungufu mkubwa katika kufuatilia habari za makundi yaliyo pembezoni na habari za vijijini kutokana waandishi kujikita zaidi kuandika habari za mijini na kuyaacha makundi mengine yakiwa hayana sauti.

“Hali hii inapaswa kubadilika ili uhuru wa habari usiwe katika maeneo maalum na kwa watu maalum bali uwe kwa wote huku makundi ya wanawake, vijana na wazee yakipata nafasi ya kupaaza sauti zao katika vyombo vya habari,” alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kufuata kwa kina maadili ya kazi zao na kuhafamu dhima na dhamana yao kwa jamii na taifa kwa ujumla. Alisema Serikali ya Zanzibar inathamini juhudi za sekta ya habari katika kuleta ufanisi na maendeleo na kwamba itaendelea kushirikiana na waandishi wa habari na kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa habari katika taasisi za serikali.

Kwa upande wake, Kaimu Waziri wa Habari, Lela Muhammed Mussa, aliwataka waandishi wa habari kutambua nafasi zao kwa kuzingatia utaalamu katika utendaji wao wa kazi ili kujitofautisha na watu wa kawaida.

Alisema hivi sasa kila mtu ni mwanahabari kwa vile anaweza kuitumia simu yake mahali popote alipo, lakini kinachohitajika kwa jamii ni kile chenye kuleta manufaa kwa umma kikiwa kimebeba sifa zote za maadili ya habari.

Vile vile, Leila aliwataka waandishi wa habari wanaochipukia kujifunza zaidi kutoka kwa wakongwe kwa lengo la kupata uzoefu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya wanahabari Zanzibar, Farouk Karim, alisema lengo kuu la kudhihirisha siku ya uhuru duniani kwa upande wa Zanzibar ni kuonyesha kuwa vyombo vya habari vilivyopo nchini vinafanya kazi kwa ushirikiano na serikali.




Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wa Mkoa wa Mjini Kichama, wakiwa katika ukumbi wa CCM Mkoa wa Mjini Amanin, wakati wa ziara ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, ambae pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa kuzungumza na kutoa shukrani kwa Viongozi wa CCM na Mabalozi wa Mkoa huo. **PICHA: IKULU**

# Othman ataka ACT-Wazalendo kushikamana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu wa Chama cha ACT-Wazalendo ambae pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wanachama wa chama hicho kushikamana kwa pamoja ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Kauli hiyo alitoa huko Shangani Mkokotoni, Wilaya ya Kaskazini A Unguja, katika kikao cha kutambulishwa kwa viongozi na wafuasi wa chama hicho.

Alisema umoja na mshikamano ndani ya chama hicho ndio uliokipa nguvu na heshima ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

“Wazee wetu walisema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu na ambapo mshikamano huo ndio uliopelekea uimara wa chama,” alisema.

Alisema mshikamano ndani ya ACT-Wazalendo imesaidia kuzuia migogoro na malumbano ndani ya chama hicho.

“Kwa sababu ya mshikamano wetu tumekuwa hatuyumbi katika kudai haki pamoja na mamlaka ya Zanzibar ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania,” alisema Othman.

Alisema Wanzanzibar na Watanzania Bara wengi wanaingia katika chama cha ACT-Wazalendo kwa kile alichokitaja kuvutiwa na ushirikiano, juhudi na dhamira njema.

Aliwataka wafuasi wa chama hicho kutoichezea dhana waliyonayo na ndio njia pekee yakufikia kule waliko kusudia kuongoza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Aidha, alisema ili kuyaenzi aliyoyaacha kiongozi wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad ni kuendeleza umoja na mshikamano alioupigania kwa miaka mingi wa uhai wake na historia ya nchi ya Zanzibar.

Mjumbe huyo wa kamati kuu alisema kuwa mshikamano umewajenga ari wanachama na kushindana na watu waliokuwa na nguvu ya dola na kueleza kuwa chama hicho kinajivunia rasilimali watu.

Sambamba na hayo alisema chama hicho kimeingia katika Serikali ya Umoja wa kitaifa (SUK) ya kuleta umoja na mshikamano bila ya kujali madhila waliyopitia kutokana na nguvu kubwa walizotumia watawala.

Naye Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji, alimtaka kiongozi huyo kuyasimamia yote aliyoyaacha Maalim Seif ambayo yana maslahi kwa Zanzibar pamoja na chama.

“Leo nakutambulisha kwa viongozi wa mikoa ninachokuomba sasa usikae nyuma tuanze kazi ya kujenga chama na kupigania haki za Wazanzibar,” alisema Duni.

Kwa upande wake, Katibu wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Salum Abdalla Bimani, alisema nchi inataka demokrasia ya kweli yenye maelewano ili nchi iweze kuneemeka kutokana na ushirikiano anamini Zanzibar itarudi kwenye hadhi yake.

## Viongozi wa dini waomba watendaji kusimamia sheria

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini Zanzibar wamewataka watendaji wa serikali kusimamia sheria wanapotekeleza majukumu yao badala ya kuvunja sheria kama walivyofanya Bodi ya udhibiti vileo baada ya kutoa vibali vinane kwa kampuni za kuigiza pombe badala ya tatu kinyume na sheria namba tisa ya vileo ya mwaka 2020.

Wito huo umetolewa na viongozi wa dini wa misikiti mitano walipokuwa wakitoa mawaidha wakati wa ibada ya Ijumaa katika Msikiti wa Mfenezini, Bububu, Kombeni, Jangombe na Kwahani, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Shekhe Mohamed Ali Amour alisema watendaji wa serikali wanatakiwa kuwa waaminifu na waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao badala ya kuwa sehemu ya wavunja sheria.

Shekhe Amour alisema Bodi ya Kudhibiti vileo Zanzibar imevunja kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Vileo baada ya kutoa vibali kwa kampuni nane za kuigiza vileo badala ya tatu.

Kwa upande wake Shekhe Abdalla Juma Mussa wa Msikiti wa Masjid Noor, alisema sheria mpya ya vileo imeweka masharti kuwa baa lazima iwe umbali wa mita 1000 kutoka eneo la huduma za jamii kama nyumba za ibada, shule hospitali au makazi.

Hata hivyo, alisema Bodi hiyo imeshindwa kuheshimu masharti ya kifungu cha 28 (K) baada ya kuendelea kutoa leseni za baa bila kuzingatia masharti ya sheria hiyo.

Kwa upande wake Shekhe Khalfan Binkhalid, aliwataka waumini kuendelea kusaidiana hasa familia zenye matatizo na kushindwa kumudu mahitaji ya chakula.

Alisema kuna watu wana umaskini wa kipato na kushindwa kumudu gharama za mahitaji ya chakula na wengine kukabiliwa na matatizo ya kifamilia ikiwamo kufiwa.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo Zanzibar, Abdulrazaki Abdulkadir, alisema waliamua kutumia busara na hekima kutoa vibali kwa kampuni zaidi ya tatu ili kulinda maslahi mapana ya mapato ya serikali.

# Askari 3 wasimamishwa Uhamiaji

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

IDARA ya Uhamiaji imewasimamisha kazi askari watatu wa Ofisi ya Uhamiaji Kurasini mkoani Dar es Salaam kwa tuhuma za kutumia nguvu dhidi ya mtuhumiwa, Alex Kyai, anayedaiwa kuwa ni tapeli.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea Mei 27, mwaka huu wakati askari hao walipomkamata mtuhumiwa huyo wa utapeli na kupokea fedha kutoka kwa wateja ili kuwapatia hati ya kusafiria kwa haraka.

Alisema mtuhumiwa huyo alikuwa ameongozana na mteja wa huduma wa hati ya kusafiria aliyemtambulisha kama mkewe.

Hata hivyo, alisema baada ya mahojiano ilibainika kuwa mtuhumiwa huyo amebainika kuwa amekuwa na tabia ya kuwalaghai na kupokea fedha kutoka kwa wateja mbalimbali ili kupata hati hiyo kwa haraka.

Alisema pia mtuhumiwa huyo amekuwa akijitambulisha kama ofisa kutoka taasisi nyeti ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema askari hao wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tukio kwa kuwa askari hao wametumia nguvu kinyume cha sheria na maadili ya kazi zao.




Ofisa Biashara Mkuu Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa NHIF, Christopher Mapunda (wapili kushoto) na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa mkoani Tanga, Shamte Said (wa kwanza kulia) wakionyesha nakala za mkataba wa makubaliano kuashiria kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa Ushirika Afya kwa wanachama wa chama hicho kilichopo katika Jiji la Tanga. Katika mpango huu Benki ya CRDB inasaidia kurahisisha upatikanaji wa bima za afya kwa wakulima waliopo katika vyama vya ushirika (AMCOS) kupitia huduma ya mkopo wa gharama za bima iliyopewa jina "Ushirika Afya Premium Loan." Wengine pichani ni viongozi wa Benki ya CRDB na NHIF.

# Wakulima 40,000 kunufaika na mradi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya OCP Afrika inayozalisha mbolea ulimwenguni, imezindua awamu ya pili ya mradi wa tathmini ya udongo na kutoa elimu kwa wakulima juu ya afya ya udongo na mbinu sahihi kwa mazao husika.

Uzinduzi ulifanyika Mei 21, 2021 Sumbawanga mjini ambapo wakulima, wasambazaji, wataalam wa kilimo na viongozi wa serikali walishiriki na Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Kalolius Misungwi, ndiye aliyefanya uzinduzi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti.

Kupitia mradi huo, wakulima baada ya kupimiwa afya ya udongo, watakutanishwa na wataalamu ili kupatiwa mapendekezo sahihi ya matumizi ya mbolea katika mashamba husika.

OCP Afrika kupitia kampuni tanzu ya OCP Tanzania ilizindua awamu ya kwanza mradi wa tathmini ya udogo mwaka 2019, na awamu ya pili ya mradi huo unatarajiwa kuhudumia wakulima na wadau wa kilimo wa mikoa minne.

Mikoa hiyo ni Rukwa, Morogoro, Mbeya na Iringa ikishirikiana na Wizara ya Kilimo, Idara za Kilimo (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kituo cha Uyole), Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mradi utatoa ushauri sahihi kwa mkulima mmoja mmoja na mapendekezo yanayolenga kuongeza tija ya mazao kama mahindi, mpunga, viazi pamoja na alizeti.

Mradi huo ni mwendelezo wa awamu ya kwanza iliyozinduliwa mwaka 2019 na kufikia wakulima na wadau wa kilimo 20,000 katika mikoa ya Njombe na Songwe.

Majibu ya utafiti wa udongo kwenye mikoa hii yameweka bayana kwamba ukiachia mbali upungufu wa madini ya Fosforas na Naitrojeni uliopo kwa kipindi kirefu, kuna upungufu pia wa madini ya Zinki, Salfa pamoja na Potasiamu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Misugwi alisema, sekta ya kilimo imeajiri namba asilimia 65 ya Watanzania wote na imelihakikishia taifa upatikanaji wa chakula kwa asilimia 100 pamoja na malighafi za viwandani.

# Homa ya nguruwe bado tishio nchini

**Na Salome Kitomari**, DODOMA

SERIKALI imesema ugonjwa wa homa ya nguruwe bado ni tishio nchini na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari, ikiwamo kutoa taarifa mapema kwa kuwa hauna kinga wala tiba.

Hayo yamo kwenye hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2021/22, iliyowasilishwa na Waziri Mashimba Mashauri, na kujadiliswa na kupitishwa na Bunge mwishoni mwa wiki.

Alisema mlipuko wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF) uliopuka kwa vipindi mbalimbali katika mwaka 2020/2021 na kusababisha jumla ya vifo vya nguruwe 5,428 katika halmashauri 18 Tanzania Bara.

"Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo hivyo nitoe wito kwa halmashauri zote nchini kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na pia pale kunapotokea mlipuko kutoa taarifa mapema kwa Wizara na kupulizia dawa ya kuua virusi ili kuzuia hasara inayoweza kuwapata wafugaji," alisema.

Alisama Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) iliandaa na kuhuisha mikakati ya kuzuia magonjwa mbalimbali yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama kwa kutumia dhana ya Afya.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mwaka 2020/2021 jumla ya ng'ombe 1,036,769, mbuzi 680,906 na kondoo 192,906 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kimeta katika mikoa ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro.

Aidha, alisema jumla ya mitamba 162,843 imechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kutupa mimba katika Wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma Jiji, Simajiro, Iringa na Njombe.

Alisema jumla ya matukio 210 ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa yalifuatiliwa na sampuli 610 zilichukuliwa ambapo mbwa 812,712 na paka 4,152 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

"Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa umeendelea kufuatiliwa kwa kukagua na kuchukuwa sampuli kwa wanyama wote wanaotupa mimba kutokana na mwaka huu kuwa na mvua nyingi," alisema.



Watangazaji wa East Africa TV na East Africa Radio; kutoka kushoto Maryam Kitosi, Deogratius Kithama, Bhoke Egina na mratibu wa mradi wa NAMTHAMINI 2021, unaoendeshwa na vituo hivyo, Sophia Mng'anya, wakizindua kampeni hiyo kwa mwaka huu katika kipindi maalum kuadhimisha Siku ya Hedhi Salama Duniani, Mei 28. Wengine ni Dk. John Relise (wa pili kulia), daktari wa magonjwa ya wanawake na meneja masoko wa kampuni ya Indo Bali, Mwanaidi Kimbeho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sendiga kumsaidia m/biashara anayedai kunyanyaswa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameahidi kumsaidia mfanyabiashara, Nassoro Lwila, wa Soko kuu Iringa, anayedai kunyanyaswa na mfanyabiashara mwenzake kwa kumvunjiwa duka lake.

Sendiga alitoa ahadi hiyo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mkoa huo.

Alisema ni wajibu wake kufanyia kazi malalamiko ya wananchi wa mkoa wake na suala hilo atalifanyia kazi.

Lwila akiwasilisha malalamiko ya wafanyabiashara sokoni hapo, alisema kodi wanayowalipa madalali wa maeneo hayo ya biashara ni Sh. 200,000 kwa mwezi huku madalali hao wakilipa halmashauri Sh. 30,000 kwa mwezi.

Aliiomba serikali kuingilia kati kwa kuwapokonya mamlaka ya kuhodhi maeneo hayo ili ikiwezekana wafanyabiashara walipe kodi halmashauri moja kwa moja.

Alisema kwa upande wake chumba alichokodishwa na dalali alivunjiwa mlango na kuchukuliwa mali zake zote na hadi sasa hajui ni wapi zimehifadhiwa.

“Naomba sana unisaidie huyu mfanyabiashara ameninyanyasa sana duka langu amevunja na mali zote amechukua na mimi nilikuwa nafanyabiashara mbali mbali ikiwamo ya huduma za kifedha,” alilalamika.

Alisema malalamiko hayo alishamfikishia aliyekuwa mkuu wa mkoa huo, Ally Hapi, ambaye aliagiza Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuchukua hatua dhidi ya malalamiko yake.

Alisema, Hapi alipinga kitendo cha maeneo ya masoko yaliyokusudiwa kutoa huduma kwa umma kuhodhiwa na watu wachache ambao wao wanalipa kodi ndogo serikalini ili kuendelea kujinufaisha kwa kodi kubwa wanayotoza wananchi.

# Fursa za kilimo cha mtama, uwele zatajwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa ya kilimo cha mtama na uwele ambacho kwa sasa mahitaji ya soko lake yameongezeka, kutokana na kutumiwa kama malighafi na viwanda vikubwa vya kutengeza bia, huku uzalishaji wake ukiwa chini.

Kauli hiyo ilitolewa na Mratibu wa Kitaifa wa Utafiti,wa mazao ya mtama, uwele na ulezi, Emanuel Mwenda, wakati wa maonyesho ya teknolojia ya mbegu bora za mazao yaliyofanyika kwenye kituo Atamizi cha kujifunzia kilimo kilichopo viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere maarufu kama Nanenane.

Mwenda ambaye pia ni mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ilonga, wilayani Kilosa Mkoani Morogoro, alisema kwa sasa mahitaji ya mtama ni tani milioni 2.1 kwa mwaka wakati uzalishaji wa wakulima nchini ni tani milioni 1.1 na asilimia 51, hivyo kuwa na upungufu wa tani 990,000

Alisema kutokana na upungufu, TARI Ilonga imeamua kuja na mbegu za teknolojia ya kisasa ikiwamo ya Masai kwa kupanda katika kituo cha Atamizi ili kuwafundisha wakulima kulima kilimo cha mtama chenye kuongeza uzalishaji kutokana na uwakika wa soko.

“Tuna mbegu ya kisasa ya mtama aina ya Masia, ambayo ni hitaji kubwa sana kwa masoko ya nchi yetu licha ya kutumika kama chakula, lakini inatumika kama malighafi kubwa kwenye viwanda vya vinywaji aina ya bia,” alisema Mwenda. Akizungumzia uwele, alisema kuna aina mbili za mbegu hizo ikiwamo Okoa na Shibe, ambazo zimepandwa katika kituo hicho kwa lengo la kuwafundisha wakulima, zina uwezo wa kutoa tani tatu kwa hekta moja na soko lake kubwa lipo Kenya kutokana na kutumika kama lishe.

Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk Joel Meliyo, alisema baada kusitishwa kwa maonyesho ya Nanenane mwaka huu wamekuja na mkakati wa vituo vyao kuendelea kutoa huduma bora za kuelimisha wakulima kulima kilimo cha kisasa na kutumia mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na watafiti.

# Kozi kwa wasaidizi wa sheria mbioni kuanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, ipo katika hatua za mwisho za uanzishaji wa kozi mpya ya wasaidizi wa sheria.

Mhadhiri na Mratibu wa Kituo cha Msaada wa Kisheria katika Taasisi hiyo, Dk. Natujwa Mvungi, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi yanayofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Alisema kozi hiyo inatarajiwa kuanza Septemba mwaka huu.

Alisema kuwa kabla ya sheria mpya, wasaidizi wa sheria walikuwa wakipewa mafunzo ya kuwajengea uwezo na taasisi mbalimbali, Lakini kwa sasa wanatambulika kisheria na ndio sababu ya kuanzisha kozi hiyo.

“Hii kozi itatolewa katika ngazi ya cheti itafundishwa kwa mwaka mmoja na itakuwa imesajiliwa chini ya Baraza la Vyuo vya Ufundi Tanzania (NACTE). Tumekuja kwenye maonyesho haya kuwaeleza wananchi na wakazi wa Dodoma tunaanzisha kozi mpya hii ambao kwa sasa wanatambulika chini ya Sheria ya Usajili wa Sheria,” alisema.

Dk. Mvungi alisema Shule ya Sheria ina kitengo cha kutoa msaada wa kisheria bure kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kulipa gharama za mawakili.

Hata hivyo, alisema kwasasa wapo Dar es Salaam, lakini wanafanya kazi na taasisi mbalimbali ikiwamo Chama cha Wanasheria (TLS) katika kusaidia wananchi kwa kutoa huduma za kisheria bure.

“Huduma hii kwa Law School hutolewa kwa siku mbili za Jumanne na Ijumaa na hutoa msaada katika maeneo mbalimbali ya kisheria na baadhi yakiwa ni mashauri ya ndoa, ardhi, mikataba na mashauri ya watoto.”

“Mfano mtu anaweza kwenda mahakamani au kesi yake hajaielewa vizuri tunamsaidia kumfafanulia au hawezi kuandaa nyaraka tunamsaidia kuziandaa au hana mwanasheria wa kwenda naye mahakamani tunaweza msaidia na kumpatia wakili,” alisema.


Alibainisha kuwa huduma hiyo imelenga kuwasaidia wananchi wasio na uwezo wa kifedha.

“Tuna vigezo vyetu vya kuwatambua na sheria inatuongoza,” alisema.

Kadhalika, alisema mwitikio wa wananchi ni mkubwa na kuwa tangu kuanzishwa huduma hiyo Februari mwaka huu, tayari wamesikiliza na kusaidia mashauri zaidi ya 200.

“Inaonyesha wananchi wameelewa kwamba tupo na tunazidi kuwaambia tupo kwa ajili yao,” alisema.

Huduma hiyo inatolewa na wahitimu wote wa Shahada ya sheria kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali ambao wanatarajia kufanya kazi kama wakili binafsi au katika utumishi nchini ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo.



# ALABA: NASUBIRI KWA HAMU KUKIPIGA MADRID

**MADRID,** Hispania

DAVID Alaba amesema anasubiri kwa hamu kubwa kucheza mechi yake ya kwanza akiwa Real Madrid baada ya kuondoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bayern Munich.

Madrid kwa sasa inatafuta kocha mpya baada ya kuondoka kwa Zinedine Zidane na ilithibitisha ujio wa Alaba akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika kule Bayern na nyota huyo wa kimataifa wa Austria amesaini mkataba wa miaka mitano na miamba hao wa LaLiga.

Baada ya kuthibitishwa Ijumaa, Alaba aliandika kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii kuzungumzia usajli huo baada ya kushinda mataji 27 akiwa na Bayern.

"Naondoka kwenye klabu ya aina yake kwenda nyingine," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, katika ukurasa wake wa Twitter.

"Baada ya miaka mingi Munich, nakwenda kupata changamoto mpya na nitafanya kila niwezalo kuhakikisha nakuwa na wakati mzuri na klabu hii mpya.

"Nasubiri kwa hamu kubwa kucheza mchezo wangu wa kwanza nikiwa na jezi nyeupe mbele ya mashabiki wa Real Madrid.

"Nina uhakika kwamba nitakuwa na wakati mzuri zaidi hapa na nitapata mafanikio makubwa na klabu hii."

# De Ligt akataa kuhusishwa Barcelona

**TURIN,** Italia

MATTHIJS de Ligt amesema hajafanya mawasiliano yoyote na Barcelona na ana furaha kucheza pale Juventus na anahisi kama "samaki majini" hapo Turin.

De Ligt alikuwa na msimu mgumu wa pili hapo Juve, akisumbuliwa na majeraha na alitumia muda mwingi akiwa benchi.

Mlinzi huyo wa kati wa Uholanzi amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo 'Bianconeri' ambako kocha wake, Andrea Pirlo amefukuzwa na nafasi yake kuchukuliwa na Massimiliano Allegri.

Barca ni miongoni mwa klabu zinazotajwa kuwania saini ya De Ligt, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, hana nia ya kusaka malisho mapya. Aliiambia ESPN: "Nina furaha kubwa hapa Juve. Nahisi kama samaki akiwa majini.

"Licha ya timu kutokuwa na kiwango kizuri, najihisi vizuri uwanjani na nakubaliana na hali ilivyo.

"Wataniruhusu niondoke? Kuna klabu nyingi ambazo zina matatizo ya kifedha, lakini unatakiwa kuiuliza klabu yenyewe."

Alipoulizwa kama Barca ndiyo inaweza kuwa kituo kinachofuata, mchezaji huyo wa zamani wa Ajax alijibu: "Sijui."






# *Depay ataka Koeman asifukuzwe Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

MEMPHIS Depay anamatumaini Barcelona watambakiza Ronald Koeman kuendelea kuwa kocha wa timu hiyo, wakati Rais Joan Laporta akionekana kutaka kutafuta mbadala wake.

Depay amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua Barcelona na sasa anataka kocha huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Koeman kuendelea kukinoa kikosi hicho.

Depay anaonekana atatua hapo akiwa mchezaji huru baada ya kuamua kuondoka Lyon na hivyo anapanga kwenda kuungana na Koeman ambaye aliiwezesha Barcelona kutwaa taji la Kombe la Mfalme [Copa del Rey].

"Nafikiri kwamba mambo yanakuwa mazuri kama unawaniwa na klabu kama Barcelona," alisema Depay. "Ni klabu ya aina yake, naamini nitakuwa na wakati mzuri wa kukaa na klabu hii.

"Lakini yote kwa yote napenda Koeman abaki na nina uhakika kwamba ataisaidia klabu."

Laporta alidokeza Ijumaa kwamba, Barcelona itatangaza usajili wa wachezaji wapya wiki hiii na Depay alithibitisha katika mahojiano na NOS kwamba "nia yangu ni kwenda pale."

HABARI MICHEZO

# Hakimi njia nyeupe PSG

**PARIS,** Ufaransa

MUDA wa Achraf Hakimi pale Inter Milan unaweza kuwa mfupi, na nyota huyo wa zamani wa Real Madrid anaweza kuhama msimu huu wa majira ya joto.

Paris Saint-Germain wamemtambua nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, kama mchezaji anayefaa kuingia na kucheza nafasi ya beki wa kulia kule Parc des Princes.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, PSG iko kwenye mazungumzo ya hali ya juu na Inter juu ya uhamisho wa Achraf, na ripoti zinaonyesha kwamba mpango huo unaweza kugharimu karibu Euro milioni 60, wakati Corriere dello Sport inasema inaweza kuwa karibu Euro milioni 70.

Achraf alikuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa Inter msimu uliopita wa majira ya joto na sasa anaweza kuwa wa kwanza kuondoka baada ya kutwaa taji la Scudetto.

Hivi karibuni Achraf alizungumza na El Chiringuito juu ya uwezekano wa kurudi kwenye klabu ya zamani ya Real Madrid na jinsi walivyoachana mwaka jana.

"Walikuwa na nafasi ya kunibakisha," alisema.

"Ninahitaji kusafisha mambo, kwa sababu watu walisema sitaki kukaa na kupigania nafasi yangu na hiyo si kweli.

"Kila mtu anajua, na mara ya mwisho kuzungumza tulisema hivi, kwamba Real Madrid ilikuwa nyumba yangu na ningependa kucheza kule, lakini kwa sababu ya hali nadhani waliamua kufanya kitu kingine."






# JUVENTUS KUMPELEKA SOKONI RAMSEY

**TURIN,** Italia

JUVENTUS inatajwa kuwa tayari kumuuza kiungo Aaron Ramsey msimu huu wa majira ya joto, baada ya sintofahamu ya hatma ya nyota huyo.

Ramsey kwa sasa yupo mazoezini na kikosi cha Wales kuelekea fainali za Mataifa ya Ulaya baada ya kucheza mechi 30 akiwa Juventus.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 30, hakuwapo kwenye kikosi cha kocha Andrea Pirlo kilichocheza mechi sita zilizopita za Serie A, pia alikosa mchezo dhidi ya Wales kwa sababu ya majeraha.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Juventus wanatarajia kumuuza Ramsey msimu wa majira ya joto wakitaka kufanya mabadiliko makubwa kikosini hapo baada ya kushindwa kutetea ubingwa wa Serie A.

Ramsey amekuwa akihusishwa na Barcelona, huku Arsenal ikitajwa kumhitaji kwa mara nyingine, ambako alikuwapo kwa takriban miaka 11 kati ya 2008 na 2019.

Tangu kiungo huyu awasili Turin kutoka Arsenal, amefanikiwa kufunga mabao sita tu katika mechi 65 alizocheza akiwa na Juve, na mkataba wake unafika mwisho mwaka 2023.

# *Kounde mlango wazi kwa Arsenal, United*

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa Sevilla, Jules Kounde, amekiri kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo wakati huu wa majira ya joto, huku Manchester United ikihusishwa naye.

Kounde ameibuka kuwa mmoja wa mabeki wa kati wanaotafutwa sana katika soko la uhamisho baada ya Dayot Upamecano kujiunga na Bayern Munich na Ibrahima Konate kukubali kutua Liverpool akitokea RB Leipzig.

Kwa muda mrefu Man United imekuwa ikihusishwa na uhamisho wa Kounde, ambaye aliisaidia Sevilla kumaliza katika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga msimu huu.

Kocha wa Man Unted, Ole Gunnar Solskjaer, ameripotiwa kuwa anatafuta beki mpya kwa ajili ya kusaidiana na Harry Maguire.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22 pia anaripotiwa kulengwa na klabu za Real Madrid, Chelsea na Arsenal.

"Kuhusu mustakabali wangu, huenda nikabadilika msimu huu wa majira ya joto," alisema Kounde akiwaambia waandishi wa habari wakati Ufaransa ikijiandaa kwa mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Wales Jumatano, kabla ya Euro 2020 inayokuja.

"Bado hakuna ukweli wowote, sijafanya uamuzi wa mwisho.

"Ni wazi, lengo langu ni kucheza siku moja katika moja ya klabu kubwa ili kuendelea kuimarika na kushinda mataji."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: UBINGWA UEFA KUNIPA MKATABA MPYA

●●● Nina uhakika kwa asilimia 100, lakini pengine tayari ninao baada ya ushindi...

**PORTO,** Ureno

THOMAS Tuchel amesema sasa anafikiri mmliki wa Cheslea, Roman Abramovich atampa mkataba mpya baada ya juzi, Jumamosi kuiwezesha timu hiyo kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Chelsea iliifunga Manchester City bao 1-0 kwenye fainali hiyo iliyopigwa katika dimba la do Dragao nchini Ureno.**

Kai Havertz alifunga bao hilo pekee katika dakika ya 42 na kuiwezesha Chelsea kubeba taji hilo.

Tuchel alijiunga na Chelsea Januari mwaka huu baada ya kufukuzwa kwa Frank Lampard.

Kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, alisaini mkataba wa miezi 18 hapo Stamford Bridge muda mfupi baada ya kufukuzwa pale Paris Saint-Germain.

Wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Tuchel alidokeza kwamba anaamini anaweza kuongeza mkataba baada ya kuipa Chelsea taji la pili la Ulaya.

"Nina uhakika kwa asilimia 100, lakini pengine tayari nina mkataba mpya baada ya ushindi. Wakala wangu alisema kitu kuhusu hili, ngoja tusubiri," alisema.

"Nilizungumza na mmiliki hapa uwanjani, ulikuwa wakati mzuri tulipoonana kwa mara ya kwanza.

"Tutazungumza zaidi na nafikiri nitakuwa na wakati mzuri zaidi nikiwa naye wiki ijayo." "Kwa uhakika kabisa nina furaha kubwa na nina matumaini ya kuendelea kuwa na klabu hii kwa muda mrefu zaidi."

## ZISIKUPITE

### RONALDO AWANIWA UNITED

MANCHESTER United inaangalia uwezekano wa kumsajili tena nyota wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo, 36, kwa kubadilishana na Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28. ***(Gazzetta dello Sport via Express)***

### ARSENAL KUMUUZA XHAKA

ARSENAL imemuambia kocha wa AS Roma, Jose Mourinho, kwamba wanataka pauni milioni 17 ili kumuachia kiungo wa Uswisi, Granit Xhaka, 28. ***(Gazzetta dello Sport)***

### SPURS WAMTAKA JESUS

KLABU ya Tottenham Hotspur ina mpango wa kumsajili nyota wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus, 24. ***(Star)***

### ATAKA KUBAKI MADRID

KIUNGO Dani Ceballos, 24, amesema anataka kubaki Real Madrid au kuondoka moja kwa moja baada ya kucheza kwa mkopo Arsenal. ***(Mail)***

### WORRALL ATAKIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 10 kwa mlinzi wa kati wa Nottingham Forest, Joe Worrall, 24. ***(Sun)***

### HODGSON ATAJWA BROM

KOCHA wa zamani wa England na Crystal Palace, Roy Hodgson anatajwa kuwaniwa na West Bromwich Albion baada ya kuondoka kwa Sam Allardyce. ***(Mirror)***

### POCHETTINO KUREJESHWA

KOCHA wa Tottenham Hotspur yupo kwenye mazungumzo na kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino ili kumrudisha klabuni hapo. ***(Sun)***

### DOUGLAS KUONDOKA VILLA

ASTON Villa inahofia kumpoteza kiungo wake nyota, Douglas Luiz, 23, huku Manchester City ikitajwa kumuwania nyota huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(90 Min)***

### SANCHO KUPEWA OFA

MANCHESTER United itatoa ofa kwa winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 21, kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mail)***

### MILAN KUMSAJILI TOMORI

AC Milan itaanza majadiliano na Chelsea ili kumsajili mlinzi, Fikayo Tomori, 23, kwa mkataba wa kudumu baada ya kucheza hapo kwa mkopo. ***(Sport Witness)***

### COULIBALY AWANIWA

KLABU ya Galatasaray imetenga pauni milioni 12.9 ili kumsajili kiungo wa Sheffield United, Ismaila Coulibaly, 20. Mchezaji huyo msimu uliopita alikuwa akicheza kwa mkopo katika klabu ya Beerschot ya nchini Ubelgiji. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

### Pamba, Transit zanukia Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE mabingwa wa zamani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Pamba SC, wamefanikiwa kusonga mbele katika hatua ya kuwania kupanda Ligi Kuu msimu ujao baada ya kupindua matokeo kwa ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Ken Gold katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi.

Katika mchezo wa kwanza ugenini, Pamba ilikubali kipigo cha mabao 2-0, hivyo sasa inasonga mbele kwa jumla ya mabao 4-3.

Timu nyingine ambayo imesonga mbele ni Transit Camp ya Dar es Salaam ambayo imewatoa mabingwa wengine wa zamani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, African Sports kwa penalti 5-4 baada ya sare ya jumla ya bao 1-1 kila timu ikishinda 1-0 nyumbani, katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Kwa matokeo hayo sasa Pamba na Transit Camp zinasubiri kujua timu zitakazomenyana nazo katika mechi ya mchujo 'Play off' kutoka Ligi Kuu ambazo zitashika nafasi ya 13 na 14 kwenye msimamo ili kuwania nafasi mbili za kupanda Ligi Kuu.

### Umisseta, Umitashumta kutikisa Mtwara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania (Umitashumta na Umisseta) yatakayoanza kutimua vumbi mkoani Mtwara Juni 6, mwaka huu.

Kuelekea mashindano hayo makatibu wakuu wa wizara tatu ikiwamo ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Habari Sanaa Utamaduni na Michezo pamoja na Tamisemi, wamekutana jijini Dodoma juzi kuweka mikakati ya kuboresha michuano hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari. Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema mashindano ya mwaka huu yatakuwa tofauti kabisa na miaka ya nyuma.

Alisema kwa ushirikiano wa wizara hizo tatu watahakikisha mashindano hayo mwaka huu yanakuwa tukio kubwa kitaifa ili kuongeza hamasa kwa vijana watakaopata fursa ya kuwakilisha shule zao.

# DILUNGA AFUNGUKA KUKATWA TAIFA STARS

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Simba, Hassan Dilunga, ambaye alihusika katika mabao yote matatu ya Simba, amesema anamshukuru kocha wake, Didier Gomes kwa kumuamini na kumpa dakika kadhaa alizocheza ambazo zimekuwa na manufaa kwake, timu nzima ya Simba, wanachama na mashabiki wote wa timu hiyo.

**Mchezaji huyo amesema hakuathirika kisaikolojia juu ya jina lake kutajwa na kuondolewa Stars kwa sababu anaamini kuwa walikosea kulitaja.**

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mechi ya Simba dhidi ya Namungo FC juzi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Dilunga ambaye siku moja kabla jina lake lilitajwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars lakini wachambuzi wengi walionekana kushangazwa na kuitwa kwake kwa madai kuwa hastahili, na ghafla ikatoka taarifa kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuwa jina lake lilikosewa na badala yake lilitakiwa kuwa la Mudathir Yahaya kutoka Azam, alisema kuwa kocha wake anamuamini na ndiyo maana baada ya mpango wa kwanza kushindikana, aliingizwa kwa ajili ya mpango wa pili ambao alichangia kufanikiwa.

"Mchezaji kukaa nje si kama ni mbovu, hujui au huna kiwango. Inawezekana umewekwa kwa sababu ya 'plan' [mpango] ya pili ya kocha. Na mimi kama mchezaji si kama ukiwekwa nje basi ubweteke, nafanya mazoezi kwa bidii, mambo ya kucheza anajua mwalimu, siku akimua akuingize uwanjani ukafanye kazi, basi unakuwa fiti unakwenda kufanya kazi kama ilivyokuwa kwenye mechi hii. Kwa hiyo kocha wetu nampongeza kwa hilo," alisema Dilunga.

Mchezaji huyo alikataa kuzungumzia sintofahamu ya jina lake kutajwa kwenye timu ya taifa, akisema kuwa kwa sababu walikosea kulitaja jina lake, basi hata yeye anaamini kuwa walikosea tu na si maana nyingine yoyote inayotafsiriwa.

"Kama walikosema basi ibaki hivyo hivyo kuwa walikosea tu," alisema.

Dilunga aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi katika kila mechi kama ilivyokuwa kwenye mechi hiyo hadi siku ya kutangazwa kuwa bingwa.

Dilunga aliingia katikati ya kipindi cha pili na kusababisha mabao yote matatu, Simba ikishinda 3-1 kwenye mechi ya hiyo ya kiporo ya Ligi Kuu Bara ambayo yote matatu walifungwa dakika 12 za mwisho.



Kikosi cha timu ya KMKM ambacho kwa sasa ni mabingwa wapya wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu wa 2020/21, baada ya juzi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi Polisi katika Uwanja wa Amaan. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# *KMKM mabingwa wapya Ligi Kuu Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mabaharia wa KMKM, imetwaa ubigwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu wa 2020/21 baada ya juzi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi katika mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Bao pekee la KMKM lililowapa ubingwa huo liliwekwa nyavuni na Mkenya Mohammed Said 'Mesi' katika dakika ya 11, ambalo lilidumu hadi kipenga cha mwisho. Matokeo hayo yaliifanya KMKM kufikisha alama 40 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote huku wakiwa na mechi mbili mkononi kabla ya ligi hiyo kumalizika.

KMKM hata kama itapoteza mechi zake mbili zilizobaki dhidi ya Chuoni na Black Sailors, matokeo hayo hayataathiri ubingwa wao kwani timu ya KVZ ambayo ipo nafasi ya pili kwenye msimamo huo, ina pointi 33, hivyo ikishinda mechi zake mbili itafikisha alama 39, moja nyuma ya mabingwa hao.

Kwa matokeo hayo, rasmi KMKM sasa imekata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu ujao wa 2021/22.

Kwa upande wa timu ya Polisi, nayo kwa sasa inapaswa kushinda michezo yake miwili iliyobaki ili kujihakikishia kubaki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao baada ya juzi kupoteza mchezo wake wa matumaini ya kusalia katika ligi hiyo.

Licha ya kupatikana bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, vita iliyopo sasa ni kwa timu zinazowania kujinasua katika janga la kushuka daraja msimu huu ambapo bado hazijajulikana kutokana na timu tano za mwisho kupishana alama moja hadi mbili, hivyo kila moja kuhitaji kushinda michezo yake miwili ya mwisho ili kujinasua katika mstari huo wa kushuka.

Michezo
Jumatatu Mei 31, 2021
Nipashe



Tuchel: Ubingwa kunipa mkataba mpya UKURASA 22

MWAKA WETU...



Nahodha wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, akinyanyua juu Kombe la Ligi Mabingwa Ulaya na kusherehekea na wachezaji wenzake baada ya kulitwaa juzi kwa kuifunga Manchester City bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Do Dragão jijini Porto, Ureno. **PICHA: MTANDAO**

# Gomes: Ubingwa sasa njia ni nyeupe Simba

## ●●● Hesabu za pointi tatu kileleni, mechi tatu mkononi zamkuna huku akifunguka...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema anaanza kuona dalili za ubingwa kwa timu yake, kwa kuwa njia ya kuelelekea huko sasa imekuwa ni nyeupe kwao.

**Simba ambayo sasa ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 64 na mechi tatu mkononi dhidi ya Yanga inayoshika nafasi ya pili na alama zake 61 baada ya kushuka dimbani mara 29, iliibuka na ushindi huo juzi katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi ikipata mabao yake dakika 12 kabla ya mechi kumalizika.**

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Gomes alisema kuongoza ligi kwa tofauti ya pointi tatu huku ukiwa na michezo mitatu mkononi, ni faida kubwa na njia nzuri ya kwenda kutwaa ubingwa kwa mara nyingine tena.

"Tuko kwenye nafasi nzuri ya ubingwa. Njia ni nyeupe baada ya ushindi. Tumepata pointi tatu, tunaongoza kwa tofauti ya pointi tatu na tuna michezo mitatu mkononi. Hii ni kuonyesha kuwa tuko kwenye njia nzuri ya kutwaa ubingwa," alisema kocha huyo.

Akiizungumzia mechi hiyo alisema haikuwa kazi rahisi kwa sababu mwanzoni mwa kipindi cha kwanza walicheza vema, lakini ugumu ulikuwa ni kwenye kufunga mabao, hadi walipotanguliwa bao ndipo mechi ilipokuwa ngumu zaidi.

"Tukafanya makosa mengi mwanzoni, lakini tuliyarekebisha kipindi cha pili. Tatizo ninaloliona ni kwamba wachezaji wangu wamecheza mechi mfululizo. Walicheza mechi ngumu na Kaizer Chiefs, halafu na Dodoma Jiji na hii, zote hizi zilikuwa ni mechi ngumu," alisema Gomes raia wa Ufaransa, ambaye kama atafanikiwa kuipa Simba ubingwa kwake itakuwa ni kwa mara ya kwanza tangu aanze kukinoa kikosi hicho Februari mwaka huu akirithi mikoba ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck aliyeachana na timu hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco, alisema wachezaji wake walipoteza umakini ilipofika dakika ya 60 na hapo kila kitu sasa kikawa upande wa Simba.

"Tulimiliki mpira kwa dakika 60, baada ya hapo tukapoteza umakini na ukicheza na timu kama Simba jinsi ilivyo kwa sasa ni lazima watakuhukumu tu.

"Yaani dakika 30 za mwisho wachezaji wangu walianza kufanya makosa mengi na Simba ina wachezaji ambao ukifanya makosa ya kujirudia, watakuadhibu tu," alisema Morocco.

Kwa matokeo hayo, Namungo inabaki nafasi ya nane, ikicheza mechi 29 zilizoiwezesha kuvuna pointi 40 hadi sasa.

# Mapinduzi arejea kuipaisha Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (pichani chini), akieleza bado ana matumaini makubwa ya kufanya vizuri katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Balama Mapinduzi, leo anatarajiwa kuanza mazoezi maalum ya uwanjani.

Yanga ambayo wachezaji wake nyota wanaandamwa na majeraha, sasa itaanza kuipata huduma ya Mapinduzi ambaye alikuwa chumba cha majeruhi kwa muda mrefu akiuguza majeraha ya mguu aliyoyapata wakati wa maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Bara msimu uliopita.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kwa mujibu wa daktari wa klabu hiyo, tayari Balama amepona na anatarajiwa kuanza mazoezi leo wakati timu ikirejea kambini. Kuhusu wachezaji wengine, ambao wapo katika chumba cha majeruhi, Saidi Ntibazonkiza, Carlos Carlinhos na Abdallah Shaibu 'Ninja', Bumbuli alisema daktari wa timu atatoa ripoti rasmi watakaporejea kambini leo.

Kwa upande wa Kocha wa timu hiyo, Nabi ametaka wachezaji wake kupambana hadi dakiza za mwisho ili kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA yanayoshikiliwa na watani zao, Simba.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >